**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# SERA YA ELIMU NA MAFUNZO 2014

**Toleo la Mwaka 2023**

RASIMU

**Mei, 2023**

# YALIYOMO


**YALIYOMO**........................................................................ i
**ORODHA YA MASUALA NA MATAMKO** ....................... iv
**VIFUPISHO** ................................................................. viii
**DIBAJI** ..............................................................................ix
**SURA YA KWANZA** ..........................................................13
**1.1. Utangulizi**....................................................................13
**1.2. Hali Ilivyo** ....................................................................15
**1.2.1. Utekelezaji wa Sera**...................................................16
**1.2.2 Upungufu wa Sera na Utekelezaji Wake**.............19
**1.2.3 Changamoto za Utoaji wa Elimu na Mafunzo** ...19
**SURA YA PILI** ....................................................................22
**FALSAFA YA ELIMU NA UMUHIMU WA SERA**............22
**2.1 Falsafa ya Elimu** .........................................................22
**2.2 Madhumuni ya Jumla ya Elimu**.............................22
**2.4 Umuhimu wa Sera** .....................................................27
**2.5 Dira, Dhima na Malengo ya Sera** ..........................27
**2.5.1 Dira** ................................................................................28
**2.5.2 Dhima**..............................................................................28
**2.5.3 Malengo ya Sera** .........................................................28
**2.5.3.1 Lengo la Jumla**.........................................................28
**2.5.3.2 Malengo Mahsusi** .....................................................28


RASMU

**SURA YA TATU** ........................................................................30
**HOJA, MASUALA NA MATAMKO YA SERA** ..................30
**3.1 Mfumo, Miundo na Taratibu Nyumbufu** ..............30
**3.2 Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo** ..............35
**3.3 Ubora wa Elimu na Mafunzo** ..................................41
**3.4 Rasilimaliwatu** ..........................................................59
**3.5 Usimamizi na Uendeshaji Madhubuti wa Elimu na Mafunzo** ..............................................................63
**3.6 Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo** ........................68
**3.7 Masuala Mtambuka katika Elimu na Mafunzo** ...70
**SURA YA NNE MUUNDO WA KISHERIA** ......................73
**4.1 Utangulizi** ....................................................................73
**4.2 Sheria za kusimamia elimu na mafunzo** .............73
**SURA YA TANO** ..............................................................76
**MUUNDO WA KITAASISI, UFUATILIAJI NA TATHMINI** ...........................................................................76
**5.1 Muundo wa Kitaasisi** ................................................76
**5.2 Mgawanyo wa majukumu** ........................................76
**5.2.1 Ngazi ya Taifa** ............................................................76
**5.2.1.1 Wizara yenye Dhamana ya Elimu na Mafunzo** ....................................................................76
**5.2.1.2 Wizara yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa** ...............................................77
**5.2.1.3 Wizara zenye Dhamana ya Sekta Nyingine** 77

**5.2.1.4 Taasisi na Mamlaka Mbalimbali za Kusimamia Utoaji wa Elimu na Mafunzo**........................78
**5.2.1.5 Taasisi na Bodi Mbalimbali za Kitaalamu**...78
**5.2.2 Ngazi ya Mkoa** ............................................................78
**5.2.3 Ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** ...............79
**5.2.4 Shule na Vyuo** ............................................................80
**5.3 Ufuatiliaji na Tathmini** ..............................................80
**5.4 Mwisho** ..........................................................................80

RASIMU

## ORODHA YA MASUALA NA MATAMKO


| MASUALA NA MATAMKO | Uk |
|---|---|
| 3.1 MFUMO, MIUNDO NA TARATIBU NYUMBUFU | 18 |
| ***(a)*** *Suala: Mfumo na muundo wa elimu na mafunzo* | 18 |
| Matamko 3.1.1– 3.1.13 | 19-21 |
| ***(b)*** *Suala: Elimu ya lazima na muda wa elimu na mafunzo* | *21* |
| Matamko 3.1.14 – 3.1.17 | 23-23 |
| **3.2 FURSA MBALIMBALI ZA ELIMU NA MAFUNZO** | 24 |
| *(a) Suala: Fursa kwa usawa katika elimu na mafunzo* | 24 |
| Matamko 3.2.1 – 3.2.3 | 24-25 |
| *(b) Suala: Usawa wa kijinsia katika elimu na mafunzo* | *25* |
| Tamko 3.2.4 | 25 |
| *(c) Suala: Elimu na mafunzo jumuishi katika ngazi zote* | *26* |
| Tamko 3.2.5 – 3.2.6 | *27* |
| *(d) Suala: Utambuzi na uendelezaji wa vipaji na vipawa katika elimu na mafunzo* | *27* |
| Tamko 3.2.7 | *28* |
| *(e) Suala: Matumizi ya teknolojia katika elimu na mafunzo* | *28* |
| Tamko 3.2.8 - 3.2.9 | *28* |
| *(f) Suala: Utambuzi wa watu waliopata ujuzi na maarifa nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo* | *29* |
| Tamko 3.2.10 | *29* |
| 3.3 UBORA WA ELIMU NA MAFUNZO | *30* |


RASIMU

| | |
|---|---|
| *(a) Suala: Uthibiti ubora wa elimu na mafunzo* | *30* |
| Matamko 3.3.1-3.4.4 | *32* |
| *(b) Suala: Mitaala ya elimu na mafunzo* | *32* |
| Matamko 3.3.5-3.3.12 | *34-35* |
| *(c) Suala: Elimu ya sayansi na teknolojia* | *35* |
| Matamko 3.3.13-3.3.15 | *37* |
| *(d) Suala: Nyenzo, vifaa, zana na mbinu za kufundishia na kujifunzia* | *37* |
| Matamko 3.3.16-3.3.21 | *38-39* |
| *(e) Suala: Miundombinu katika taasisi za elimu na mafunzo* | *39* |
| Tamko 3.3.22 | *40* |
| *(f) Suala: Mazingira salama na rafiki na huduma muhimu katika taasisi za elimu* | *40* |
| Matamko 3.3.23-3.3.24 | *41* |
| *(g) Suala: Ushauri na unasihi katika elimu na mafunzo* | *41* |
| Tamko 3.3.25 | *42* |
| *(h) Suala: Elimu yenye kudumisha uzalendo na amani* | *42* |
| Matamko 3.3.26-3.3.27 | *43* |
| *(i) Suala: Matumizi ya Kiswahili, Kiingereza, lugha nyingine za kigeni na Lugha ya Alama ya Tanzania katika mawasiliano* | *43* |
| Matamko 3.3.28-3.3.29 | *45* |
| *(j) Suala:Lugha ya kufundishia* | *45* |
| Matamko 3.3.30-3.3.32 | *46* |
| *(k) Suala: Upimaji na tathmini ya maendeleo ya* | *47* |




RASIMU

| | |
|---|---|
| *wanafunzi katika elimu na mafunzo* | |
| Tamko 3.3.33 | *47* |
| 3.4 RASILIMALIWATU | *48* |
| ***(a)*** *Suala: Upatikanaji wa walimu, wakufunzi na wahadhiri mahiri kwa ajili ya sekta ya elimu* | *48* |
| Matamko 3.4.1-3.4.9 | *49-50* |
| ***(b)*** *Suala: Upatikanaji wa rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha kwa maendeleo ya taifa* | *50* |
| Matamko 3.4.10-3.4.11 | *51* |
| 3.5 USIMAMIZI NA UENDESHAJI MADHUBUTI WA ELIMU NA MAFUNZO | *51* |
| ***(a)*** *Suala: Uongozi, usimamizi na uendeshaji fanisi katika sekta ya elimu* | *51* |
| Matamko 3.5.1-3.5.4 | *52-53* |
| ***(b)*** *Suala: Ushirikiano katika elimu na mafunzo kati ya Tanzania Bara na Zanzibar* | *53* |
| Tamko 3.5.5 | *54* |
| ***(c)*** *Suala: Ushirikiano katika elimu na mafunzo kikanda na kimataifa* | *54* |
| Matamko 3.5.6-3.5.7 | *55* |
| ***(d)*** *Suala: Upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya maendeleo ya elimu na mafunzo* | *55* |
| Matamko 3.5.8-3.5.9 | *56* |
| ***(e)*** *Suala: Upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi za elimu na mafunzo* | *56* |
| Matamko 3.5.10-3.5.11 | *57* |
| 3.6 UGHARIMIAJI WA ELIMU NA MAFUNZO | *57* |
| *(a) Suala: Ugharimiaji endelevu wa elimu na mafunzo* | *57* |

| | |
|---|---|
| Matamko 3.6.1-3.6.2 | *58* |
| 3.7 MASUALA MTAMBUKA KATIKA ELIMU NA MAFUNZO | *58* |
| *(a) Suala: Elimu ya mazingira* | *58* |
| Tamko 3.7.1 | *59* |
| *(b) Suala: Magonjwa mbalimbali* | *59* |
| Tamko 3.7.2 | *60* |
| *(c) Suala: Ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi katika utoaji wa elimu na mafunzo* | *60* |
| Matamko 3.7.3-3.7.4 | *60-61* |
| | |


RASIMU

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| LAT | Lugha ya Alama ya Tanzania |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| SADC | Southern Africa Development Community |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organisation |

RASIMU

# DIBAJI

Serikali imekusudia kuleta mapinduzi ya kijamii na kiuchumi ili kuibadili Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Sekta ya elimu na mafunzo, kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na Mpango wa muda mrefu wa Maendeleo ya Taifa 2011/12 hadi 2024/25, inatarajiwa kuleta maendeleo ya rasilimaliwatu kwa kutayarisha Watanzania mahiri walioelimika na wapendao daima kujielimisha ili kuliletea Taifa maendeleo na kuliweka kwenye uchumi shindani. Ili kufikia lengo hilo, mfumo wa elimu na mafunzo unaotumika nchini lazima utoe fursa za kutosha kwa watu wengi zaidi kuelimika na kuendelea kujielimisha. Kadhalika, mfumo huu unawajibika kutoa elimu na mafunzo yenye ubora unaokubalika na kutambulika kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kufanikisha hili, Serikali imekuwa ikitekeleza mipango na programu mbalimbali za elimu na mafunzo. Hata hivyo, katika kipindi cha utekelezaji wa Sera cha 2015-2022, changamoto mbalimbali zimekuwa zikichangia katika kushuka kwa ubora wa elimu na mafunzo nchini. Changamoto hizo ni pamoja na udhaifu katika mfumo na muundo wa elimu na mafunzo; uhaba wa walimu; uhaba wa zana, nyenzo, vifaa na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia; na mapungufu katika ithibati na uthibiti wa ubora wa shule na vyuo.

Toleo la Sera la mwaka 2023 linabainisha masuala ambayo Serikali, kwa kushirikiana na wadau katika elimu na mafunzo, itayawekea mkazo zaidi ili kuweka mazingira mazuri ya kufikia malengo ya

mipango ya maendeleo. Masuala haya ni pamoja na kuinua ubora wa mfumo wa elimu na mafunzo ili uwe na tija na ufanisi, kutoa fursa za elimu na mafunzo kwa usawa na kuendelea kuinua ubora wa mitaala ya elimu na mafunzo kukidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa. Aidha, Serikali itaendeleza matumizi ya lugha za Kiswahili, Kiingereza na Alama, pamoja na lugha nyingine za kigeni katika elimu na mafunzo. Vilevile, itaendelea kuinua ubora wa mfumo wa upimaji, tathmini na utoaji vyeti katika ngazi zote, ikiwa pamoja na utoaji wa ithibati za ujuzi katika ngazi mbalimbali. Serikali itaimarisha uwezo wa uongozi na utawala katika sekta ya elimu na mafunzo na kupanua wigo wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo.

Dira ya elimu na mafunzo nchini ni *"Kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye umahiri ikiwemo maarifa, stadi, uwezo na mtazamo chanya utakaomwezesha kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa"*. Vilevile, Dhima ya Sera ni *"Kuinua ubora wa elimu na mafunzo kwa kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya taifa".* Ili kufanikisha utekelezaji wa Sera hii kwa ukamilifu, kunahitajika ushiriki wa wadau wote wa elimu na mafunzo katika ngazi zote, zikiwemo sekta binafsi, Asasi za Kiraia na washirika wengine wa maendeleo.

Napenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika mchakato mzima wa kukamilisha toleo hili la pili la Sera ya Elimu na Mafunzo.

RASIMU

Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb.)
**Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia**

RASIMU

RASIMU

# SURA YA KWANZA
# USULI

## 1.1. Utangulizi

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Sera), Toleo la Mwaka 2023, ni matokeo ya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014. Sera hiyo nayo ilitokana na matokeo ya mapitio yaliyofuta *Sera ya Elimu na Mafunzo* (1995), *Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo* (1996), *Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu* (1999) na *Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Elimu Msingi* (2007). Sera hizo, kwa ujumla, zilitoa mwongozo kuhusu kuongeza ushirikishwaji wa sekta binafsi; kuongeza usawa katika fursa za elimu na mafunzo; kupanua wigo wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo; kuhuisha muundo wa uongozi wa elimu kwa kupeleka madaraka na majukumu katika ngazi ya shule, jamii, halmashauri, na mikoa; kuinua ubora wa elimu; kuimarisha uhusiano kati ya elimu rasmi na elimu isiyo rasmi na kukuza utamaduni wa elimu ya kujiajiri na kubuni ajira.

Sera 2014 ilizingatia mahitaji ya kimaendeleo kikanda na kimataifa, mabadiliko ya sera za jumla na mipango ya kitaifa iliyojitokeza katika kipindi hicho. Kutokana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda mrefu 2011/12 hadi 2024/25, Serikali imelenga kujenga jamii iliyoelimika na yenye kupenda kujielimisha. Pamoja na azma hiyo, Tanzania imeridhia Itifaki ya SADC (Southern Africa Development Community) (1997) kuhusu elimu na mafunzo inayozitaka nchi wanachama kuwa na elimu ya lazima kwa kipindi kisichopungua miaka tisa; Itifaki ya Dakar (2000) kuhusu Elimu kwa wote; Makubaliano ya Perth UNESCO (United Nations Educational, Scientific and Cultural Organisation) (2007) kuhusu Elimu ya Sayansi

na Teknolojia na mafunzo ya ufundi; na Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tangu kuzinduliwa kwa Sera 2014, takribani miaka minane imepita. Katika kipindi hicho, masuala kadhaa yametekelezwa, ikiwemo uwekezaji katika sekta ya elimu na mafunzo, hususan katika miundombinu ya madarasa na maabara, na vitendea kazi muhimu ikiwemo vitabu vya kiada.

Hata hivyo, sera za jumla, mikataba ya kikanda na kimataifa na maoni mbalimbali ya wadau vimekuwa vikihoji utoshelevu wa Sera 2014. Hivi vyote vimeonesha uhitaji wa maboresho ya elimu na mafunzo nchini ili kuendana na mahitaji ya sasa na baadaye; hususan katika kukuza ujuzi, maarifa na weledi ili wahitimu katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo waweze kuendana na mahitaji ya ulimwengu wa kazi na maisha kwa ujumla. Hivyo, Toleo la Mwaka 2023 la Sera 2014, limejumuisha masuala mbalimbali yaliyojitokeza tangu Sera ilipozinduliwa mwaka 2015 ili kutoa mwelekeo mpya.

Sera 2014, Toleo la Mwaka 2023, imezingatia utatuzi wa changamoto za kielimu ili kuendana na mipango ya kitaifa na mahitaji ya kikanda na kimataifa. Mwelekeo mpya wa elimu na mafunzo nchini unazingatia mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia. Hivyo, Sera imejikita katika hoja zifuatazo: kuimarisha mfumo nyumbufu utakaomwezesha Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali; kuinua ubora wa elimu na mafunzo; kuongeza fursa za elimu na mafunzo; kuandaa na kuongeza rasilimaliwatu kuendana na vipaumbele vya Taifa; kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo; kuweka mfumo endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo; na kuwa na mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia masuala mtambuka.

`

## 1.2. Hali Ilivyo

Sekta ya elimu na mafunzo ina jukumu la kuandaa na kuzalisha rasilimaliwatu kwa ajili ya Taifa. Taarifa mbalimbali zinaonesha kwamba kuna nakisi kubwa ya wataalamu wa kiwango cha juu wa kukidhi matakwa ya uchumi wa kati. Takwimu linganifu zinaonesha kuwa rasilimaliwatu ya Tanzania kwa kiasi kikubwa bado ni ya wafanyakazi wenye ujuzi wa chini kwa asilimia 84, wakifuatiwa na wenye ujuzi wa kati kwa asilimia 13 na wenye ujuzi wa juu kwa asilimia tatu. Ulinganifu unaonesha kuwa kwa nchi za kipato cha kati ngazi ya chini, wastani wa rasilimaliwatu yenye ujuzi wa chini huwa asilimia 55, ujuzi wa kati huwa asilimia 33 na ujuzi wa juu asilimia 12. Hivyo, sekta ya elimu na mafunzo ina changamoto ya kuinua uwiano wa wafanyakazi wenye ujuzi katika fani mbalimbali ili kufikia mahitaji ya rasilimaliwatu kwa nchi ya kipato cha kati.

Mfumo wa elimu na mafunzo uliopo una changamoto ya kuliwezesha Taifa kukidhi ongezeko la mahitaji ya rasilimaliwatu kulingana na vipaumbele vya Taifa. Takwimu zinaonesha kuwa Tanzania inatoa wahitimu wachache wa elimu ya juu ukilinganisha na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community) na za Jumiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Aidha, mfumo wa elimu unahamasisha njia moja tu ya kumwezesha mwanafunzi kupata elimu hadi kiwango cha juu, nayo ni kuwa kila kijana anayeanza darasa la kwanza anatakiwa aendelee na elimu hiyo hadi kufikia chuo kikuu. Mkengeuko wowote kutoka kwenye njia hii unachukuliwa na jamii kama dalili ya mwanafunzi kushindwa. Ukweli ni kwamba siyo kila kijana ana

nia au uwezo wa kufuata njia hiyo. Aidha, uchumi wa nchi nyingi duniani unaoendeshwa kwa ufanisi unategemea uwiano wa rasilimaliwatu yenye ujuzi mchanganyiko. Kwa hali hiyo, ni dhahiri kuwa Taifa linahitaji kuongeza kasi ya kuandaa wataalamu mahiri kuendana na vipaumbele vyake kwa kuongeza fursa na kuinua ubora wa elimu na mafunzo.

### 1.2.1. Utekelezaji wa Sera

Katika kipindi cha miaka minane cha utekelezaji wa Sera, Serikali ilijikita katika kuongeza fursa na ubora wa elimu na mafunzo. Kuanzia mwaka 2016, Serikali ilianza kutoa elimu ya msingi na sekondari ya chini bila ada; na mwaka 2020 ilianza kutoa elimu ya sekondari ya juu bila ada. Pia, Serikali imeendelea kuongeza kiasi na viwango vya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Aidha, Serikali imeondoa vikwazo vinavyozuia wanafunzi walioacha masomo kwa sababu mbalimbali, kurejea shuleni na kukamilisha mzunguko wa elimu katika ngazi husika. Sambamba na hayo, Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kuboresha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya makundi yote katika ngazi zote za elimu.

Utekelezaji wa afua hizo umeleta mafanikio mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa:

a. Miundombinu katika shule za awali, msingi na sekondari: madarasa ya elimu ya awali kwa shule za msingi kuongezeka kutoka 16,889 mwaka 2015 hadi kufikia 19,284 mwaka 2022, sawa na asilimia 14.2; idadi ya shule za msingi kuongezeka kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 19,261 mwaka 2022, sawa na asilimia 14; na idadi ya shule za

sekondari kuongezeka kutoka 4,708 mwaka 2015 hadi 5,540 mwaka 2022, sawa na asilimia 17.7;

b. Idadi ya vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 672 mwaka 2015 hadi 830 mwaka 2021, sawa na asilimia 23.5.

c. Idadi ya vyuo vya elimu ya juu kutoka 50 mwaka 2013/14 hadi 52 mwaka 2020/21, sawa na asilimia 4..

d. Idadi ya wanafunzi katika elimu ya awali kutoka 1,066,823 mwaka 2015 hadi 1,543,843 mwaka 2022, sawa na asilimia 44.7;

e. Idadi ya wanafunzi katika elimu ya msingi kutoka 8,298,282 mwaka 2015 hadi 11,420,973 mwaka 2022, sawa na asilimia 37.6;

f. Idadi ya wanafunzi katika elimu ya sekondari ya chini kutoka 1,648,359 mwaka 2015, hadi 2,645,115 mwaka 2022 sawa na asilimia 60.5;

g. Idadi ya wanafunzi katika elimu na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 130,079 mwaka 2016/17 hadi 141,458 mwaka 2021/22, sawa na asilimia 8.7;

h. Idadi ya wanafunzi waliojiunga na elimu ya ufundi sanifu kutoka 128,121 mwaka 2016/17 hadi 179,518 mwaka 2021/22, sawa na asilimia 40.1;

i. Idadi ya wanufaika wa mikopo katika elimu ya juu kutoka

121,329 mwaka 2017/18 hadi 177,893 mwaka 2021/22 sawa na asilimia 46.6;

j. Idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka 162,510 mwaka 2012/13 hadi 295,919 mwaka 2021/22, sawa na asilimia 82.1.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Sera, bado kuna upungufu unaoathiri ubora wa elimu na mafunzo yatolewayo. Upungufu huo ni pamoja na:

a. Uhaba wa miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ikiwemo vitabu, maabara, maktaba na madarasa, na kumbi za mihadhara. Kwa mfano, katika mwaka 2022, uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi katika elimu ya msingi ulikuwa 1:2 na elimu ya sekondari 1:3, ukilinganisha na uwiano stahiki wa 1:1; uwiano wa darasa kwa wanafunzi katika elimu ya msingi ulikuwa 1:70 ukilinganisha na uwiano stahiki wa 1:45; na katika elimu ya sekondari ya chini ulikuwa 1:36 ukilinganisha na uwiano stahiki wa 1:35;

b. Uhaba wa walimu hususan katika masomo ya sayansi, amali, lugha na hisabati. Kwa mfano, kwa takwimu za mwaka 2021/22, shule za sekondari zilikuwa na upungufu wa walimu 12,577 wa somo la fizikia, walimu 13,686 wa somo la hisabati, walimu 12,027 wa somo la bailojia, na walimu 10,600 wa somo la kemia. Katika elimu ya juu, takwimu za mwaka 2021/22 zinaonesha kuna upungufu wa wanataaluma 3,639.

### 1.2.2 Upungufu wa Sera na Utekelezaji Wake

Sera haikutoa ufafanuzi wa kutosha na hivyo kutoa mwanya wa tafsiri tofauti katika baadhi ya maeneo ya msingi kama vile muundo wa elimu, elimu ya amali na lugha ya kufundishia. Aidha, Sera haikutoa umuhimu wa kutosha katika baadhi ya maeneo ya msingi, yakiwemo elimu ya ualimu, elimu ya juu, utafiti katika elimu na ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa elimu na mafunzo.

Hata hivyo, elimu bila ada kwa wanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari katika mfumo wa umma ndilo eneo la msingi la Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 lililotekelezwa. Maeneo mengine ya msingi ya Sera hayakutekelezwa.

### 1.2.3 Changamoto za Utoaji wa Elimu na Mafunzo

Jukumu kuu la sekta ya elimu ni kuzalisha nguvukazi ya kutosha na yenye umahiri na weledi stahiki katika ngazi mbalimbali na katika uwiano stahiki kwa maendeleo ya Taifa. Katika jitihada za kutekeleza jukumu hilo, sekta inakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwemo:

a. Upungufu wa nguvukazi ya kutosha iliyoelimika. Changamoto hii inatokana na:

   i. Kutokuwepo kwa mfumo fanisi wa kubainisha mahitaji ya nguvukazi ya jumla na ya kimkakati inayohitajika katika sekta mbalimbali na kwa ajili ya ajenda ya maendeleo ya nchi.

   ii. Upungufu wa rasilimalifedha ya kuwezesha ugharimiaji wa

RASIMU

elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu. Hili linatokana na kukosekana kwa mfumo fanisi, endelevu na jumuishi wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo ili kukidhi mahitaji katika ngazi zote.

iii. Kutokuwepo kwa mfumo endelevu wa utambuzi wa sifa za elimu na ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi utakaowawezesha watu kujiendeleza kielimu na kuingia katika ulimwengu wa kazi.

iv. Kutokuwepo kwa utaratibu wa utambuzi na uendelezaji wa wanafunzi wenye vipaji na vipawa, mahitaji maalumu na mazingira duni ya kujifunzia.

b. Upungufu wa nguvukazi yenye umahiri na weledi. Changamoto hii inatokana na:

i. Mitaala katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kutokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia na hivyo kutoa wahitimu ambao hawana umahiri wa kutosha kujiajiri au kuajiriwa;

ii. Kutokuwepo kwa mfumo thabiti wa uthibiti na ithibati ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu.

iii. Uwezo hafifu wa wahadhiri katika taasisi za elimu ya juu kuzalisha maarifa yanayoendana na mahitaji ya jamii.

c. Upungufu wa nguvukazi yenye uwiano stahiki wa kiujuzi. Changamoto hii inatokana na kutokuwa na mfumo nyumbufu wa elimu na mafunzo unaomwezesha Mtanzania

RASIMU

kujiendeleza kulingana na mahitaji, sehemu, na mazingira yake.

d. Usimamizi wa utoaji wa elimu na mafunzo usiokuwa na tija. Changamoto hii inatokana na uratibu usioridhisha katika utoaji wa elimu na mafunzo unaotokana na sheria, kanuni, taratibu, miongozo na mwingiliano wa majukumu baina ya taasisi.

Kutokana na changamoto hizo, Serikali iliamua kufanya mapitio ya Sera 2014. Matokeo ya mapitio hayo ni Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023 ambayo inatoa mwongozo wa utoaji wa elimu itakayoandaa rasilimaliwatu ya kutosha na yenye uwezo na maarifa ya kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa.

RASIMU

RASIMU

# SURA YA PILI
# FALSAFA YA ELIMU NA UMUHIMU WA SERA

## 2.1 Falsafa ya Elimu

Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea itaendelea kuongoza utoaji wa elimu na mafunzo kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea kitaifa na kimataifa katika nyanja za siasa, jamii, uchumi, sayansi na teknolojia.

## 2.2 Madhumuni ya Jumla ya Elimu

Madhumuni ya elimu na mafunzo nchini ni kama ifuatavyo:

a. Kukuza na kujenga haiba ya Mtanzania ili aweze kubadili maisha yake na kuchangia katika maendeleo ya jamii, Taifa na dunia;

b. Kukuza uelewa na kuthamini utamaduni, mila na desturi za Watanzania, kuheshimu tofauti za kitamaduni, na kuwa na mitazamo chanya;

c. Kumwezesha Mtanzania kukuza na kutumia kwa ustahiki, stadi za teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano na mawasiliano katika kujiletea maendeleo binafsi na ya taifa kwa ujumla;

d. Kuendeleza na kukuza kujiamini, kudadisi, weledi na heshima kwa utu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya taifa;

e. Kukuza na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, mtazamo chanya, uhodari, ujasiriamali, weledi na kuwezesha utamaduni unaothamini maendeleo ya binadamu ili kukidhi mahitaji halisi ya jamii;

f. Kumwezesha Mtanzania kuelewa, kulinda na kuendeleza misingi ya maadili ya taifa na uadilifu ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji, pamoja na kuthamini haki za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;

g. Kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi ili kuboresha utendaji kazi katika sekta mbalimbali ikiwemo matumizi ya teknolojia na ubunifu;

h. Kukuza ushirikiano wa kitaifa, kikanda, na kimataifa; amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia;

i. Kuimarisha uwajibikaji wa pamoja katika kuboresha afya na ustawi wa watu na jamii, usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira;

j. Kukuza fursa za elimu isiyo na ukomo kwa watu wote kwa kuzingatia matendo jumuishi, haki, kujisimamia, kujali na kutoa afua stahiki kwa jamii; na

k. Kuwezesha ujenzi wa ujuzi ili kuchochea mafanikio katika ulimwengu wa kazi na mafunzo ya kitaalamu.

### 2.3 Madhumuni ya Elimu kwa kila Ngazi ya Elimu

Madhumuni ya elimu na mafunzo nchini kwa kila ngazi ni kama ifuatavyo:

### 2.3.1 Elimu ya Awali

a. Kumwandaa mtoto kimakuzi, kimwili, kiakili, kimaadili, kijamii na kijinsi;

b. Kubaini mtoto mwenye mahitaji maalumu na kumpa fursa stahiki;

c. Kumwezesha mtoto kumudu lugha mbalimbali;

d. Kumwandaa mtoto kujiunga na elimu ya msingi.

### 2.3.2 Elimu ya Msingi

a. Kumwandaa mwanafunzi kuwa na stadi za kusoma, kuandika, na kuhesabu;

b. Kumjengea mwanafunzi uwezo wa kuwasiliana kwa lugha fasaha, ikiwemo lugha ya Taifa ya Kiswahili, lugha za kigeni, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha ya mguso;

c. Kumjengea mwanafunzi misingi ya uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria;

d. Kumwezesha mwanafunzi kutambua, kuheshimu na kudumisha utamaduni wa Mtanzania na umoja wa kitaifa, na kutambua tamaduni nyingine;

e. Kumjengea mwanafunzi ubunifu, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, na kutatua matatizo;

f. Kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa;

g. Kumwezesha mwanafunzi kutambua na kutumia sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano katika kujifunza na maisha ya kila siku;

h. Kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuimarisha na kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na

i. Kumtayarisha mwanafunzi kuendelea na elimu ya sekondari.

### 2.3.3 Elimu ya Sekondari

a. Kuimarisha, kupanua na kuendeleza maarifa, stadi, na mtazamo chanya uliopatikana katika ngazi ya elimu ya msingi;

b. Kumwezesha mwanafunzi kuelewa na kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, tunu za Taifa na demokrasia; na kuthamini haki za binadamu na wajibu unaoendana na haki hizo;

c. Kumwezesha mwanafunzi kujisomea, kujiamini, kujiendeleza kwenye nyanja za sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, kiufundi, kikazi na kiujasiriamali;

RASIMU

d. Kumwezesha mwanafunzi kutumia stadi za lugha, ikiwemo Lugha ya Taifa ya Kiswahili, LAT, Lugha Mguso, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni;

e. Kumwezesha mwanafunzi kutambua uwajibikaji wa pamoja wa kutunza afya, kuthamini usawa wa kijinsia na kusimamia utunzaji endelevu wa mazingira;

f. Kuimarisha misingi ya uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria; na

g. Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha mhitimu kujiunga na elimu ya juu na mafunzo ya amali sanifu baada ya elimu ya sekondari, kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia mazingira yake.

### 2.3.4 Elimu ya Juu

a. Kuimarisha, kupanua, na kuendeleza maarifa, stadi, na mtazamo chanya uliopatikana kabla ya kujiunga na elimu ya juu;

b. Kumwezesha mwanafunzi kupata maarifa na stadi za juu za kitaaluma na kitaalamu;

c. Kuandaa wanataaluma na wataalamu kwa ajili ya sekta mbalimbali;

d. Kuimarisha misingi ya uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria;

RASIMU

e. Kujenga uwezo wa wanataaluma na taasisi za elimu ya juu katika kutoa na kuendeleza maarifa mapya kupitia utafiti, machapisho yenye ubora na kutatua changamoto za kijamii.

### 2.4 Umuhimu wa Sera

Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023 imetokana na hoja mbalimbali za wadau zilizotolewa tangu Sera ilipozinduliwa mwaka 2015. Toleo hili limefanya marekebisho na maboresho katika maeneo ya Sera yaliyobainika kuwa na upungufu na kuongeza maeneo ambayo hayakuzingatiwa, pamoja na kutoa ufafanuzi katika maeneo yaliyokuwa yanaleta mkanganyiko katika tafsiri. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na muundo wa elimu, elimu ya amali, elimu ya ualimu, elimu ya juu, utafiti katika elimu, lugha ya kufundishia na ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa elimu na mafunzo.

Lengo la maboresho hayo ni kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo ili Taifa liweze kuzalisha wahitimu wenye umahiri wa msingi katika mawasiliano, ushirikiano, ubunifu, fikra tunduizi, utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijitali, maadili na uzalendo. Hizi zote ni Stadi za Karne ya 21. Kwa kuzingatia Stadi hizo, maboresho hayo yatawafanya wahitimu kuweza kumudu ushindani wa kitaifa, kikanda na kimataifa na hivyo kukidhi mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia na kiuchumi duniani.

### 2.5 Dira, Dhima na Malengo ya Sera

Msingi wa elimu na mafunzo utaendelea kujikita katika kumjengea Mtanzania misingi bora ya malezi, maadili, ujuzi, umahiri na

RASIMU

kumwezesha kujitegemea kwa kuzingatia yafuatayo:

### 2.5.1 Dira

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika, mwenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaomwezesha kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa.

### 2.5.2 Dhima

Kuinua ubora wa elimu na mafunzo kwa kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika, wenye stadi na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa.

### 2.5.3 Malengo ya Sera

#### 2.5.3.1 Lengo la Jumla

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika, mwenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaomwezesha kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa.

#### 2.5.3.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya Sera ni kuwa na:

a. Mfumo, muundo na taratibu nyumbufu kumwezesha kila Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali kitaaluma na kitaalamu;

b. Usimamizi na uendeshaji madhubuti wa elimu na mafunzo nchini;

RASIMU

c. Mfumo wezeshi wa kujenga ufanisi na ushindani katika elimu ya juu;

d. Elimu na mafunzo yenye viwango vya ubora unaotambulika kitaifa, kikanda na kimataifa;

e. Rasilimaliwatu ya kutosha na yenye umahiri na weledi stahiki kuendana na vipaumbele vya Taifa;

f. Mtanzania mwenye utamaduni wa kupenda kujisomea na kujiendeleza katika muktadha wa elimu bila ukomo;

g. Mfumo endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo nchini; na

h. Mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia masuala mtambuka.

RASIMU

# SURA YA TATU
# HOJA, MASUALA NA MATAMKO YA SERA

## 3.1 Mfumo, Miundo na Taratibu Nyumbufu

Mfumo, miundo na taratibu nyumbufu zinalenga kumwezesha kila Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali kitaaluma na kitaalamu. Hoja hii imejikita katika masuala yafuatayo:

### (c)Suala: Mfumo na muundo wa elimu na mafunzo

**Maelezo**

Serikali imewezesha upatikanaji wa fursa ya elimu kwa watoto wa jinsi zote kwa kuandikisha asilimia 108.5 ya wanafunzi katika elimu ya msingi mwaka 2022. Hata hivyo, elimu baada ya elimu ya msingi imeendelea kuwa na changamoto mbalimbali kwa sababu mfumo uliopo sasa bado unategemea zaidi utaratibu wa kuchuja wanafunzi kwa ajili ya kuendelea na masomo, badala ya kutoa fursa ya kuwaendeleza kadri ya uwezo, vipaji na vipawa vyao. Mfumo huu pia, kwa kiwango kikubwa umejikita katika taaluma pekee, na hivyo kuwafanya wale wanaoshindwa kuendelea kitaaluma na kuchaguliwa kujiunga na elimu na mafunzo ya amali kuonekana wamefeli. Hiki ni kiashiria cha mfumo kutokuwa nyumbufu na hivyo kushindwa kutoa fursa anuai za elimu na mafunzo ambazo zinaweza kumfanya kila mwanafunzi kupata ujuzi na maarifa kwa ajili ya ulimwengu wa kazi kulingana na uwezo, matakwa na malengo yake. Katika muktadha huo, mfumo nyumbufu wa elimu unahitajika.

Katika muundo wetu wa elimu wa 2+7+4+2+3+ mwanafunzi anayeanza masomo akiwa na umri wa miaka 7 atahitimu elimu ya juu akiwa na umri mkubwa, takribani miaka 25, ikilinganishwa na nchi kama za Afrika ya Kusini, Maurishasi, Malesia na Ufini ambapo umri wa kijana anayemaliza elimu ya juu ni takribani miaka 20 hadi 22. Kwa sababu hii, umri wa kuanza darasa la kwanza umepunguzwa kutoka miaka saba hadi sita, kama ilivyo katika nchi nyingi duniani. Vilevile, muundo uliorekebishwa unaruhusu mwanafunzi kukamilisha mzunguko wa masomo kwa muda mfupi zaidi.

**Madhumuni**

Kuwa na mfumo nyumbufu wa elimu na mafunzo wenye tija na ufanisi na hivyo kuongeza idadi ya wananchi walioelimika na mahiri katika fani mbalimbali kuendana na mahitaji ya Taifa na ulimwengu wa kazi.

## MATAMKO

*3.1.1 Serikali itaweka mfumo nyumbufu wa elimu na mafunzo ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kujielimisha na kuwa huru kutafuta elimu katika fani wanayopenda, kulingana na stahili na uwezo wao.*

*3.1.2 Mfumo wa elimu utajikita katika kujenga umahiri, ambapo msisitizo utakuwa katika kupata ujuzi, maarifa, weledi, mwelekeo, mitazamo chanya, maadili na tabia stahiki kulingana na mahitaji ya taifa na ulimwengu wa kazi.*

*3.1.3 Elimu katika mfumo rasmi itagawanyika katika ngazi za elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari na elimu*

*ya juu.*

*3.1.4 Muundo katika mfumo rasmi wa elimu na mafunzo utakuwa 1+6+4+2/3+3+, kwa maana ya mwaka mmoja wa elimu ya awali, miaka sita ya elimu ya msingi, miaka minne ya elimu ya sekondari ngazi ya chini, miaka miwili ya elimu ya sekondari ngazi ya juu au miaka mitatu ya amali sanifu, na miaka isiyopungua mitatu ya elimu ya juu.*

*3.1.5 Elimu ya awali italenga kumwaandaa mtoto kimwili, kijamii, kihisia, na kiakili ili kumwezesha kuishi na jamii na kujiunga na elimu ya msingi.*

*3.1.6 Elimu ya lazima itajumuisha elimu ya msingi na elimu ya sekondari ngazi ya chini na itatolewa kwa miaka 10.*

*3.1.7 Elimu ya msingi itakuwa elimu ya jumla kama itakavyofafanuliwa kupitia mitaala husika.*

*3.1.8 Elimu ya sekondari ngazi ya chini itagawanyika katika mikondo miwili ambayo ni mkondo wa elimu ya jumla, na mkondo wa elimu ya amali.*

*3.1.9 Elimu ya amali itakuwa sehemu muhimu ya mfumo wa elimu na itatolewa kulingana na mitaala ya ngazi husika.*

*3.1.10 Elimu ya sekondari ngazi ya juu au elimu ya amali sanifu itakuwa hitaji la msingi kwa ajili ya kujiunga na elimu ya juu.*

*3.1.11 Elimu ya juu itakuwa elimu baada ya elimu ya sekondari na itagawanyika katika mkondo wa elimu ya jumla na elimu ya*

RASIMU

*amali.*

3.1.12 *Elimu nje ya mfumo rasmi itatambuliwa na watakaopitia mfumo huo watakuwa na fursa ya kujiunga na mfumo rasmi wa elimu kulingana na vigezo vitakavyowekwa.*

3.1.13 *Serikali itaweka na kusimamia mfumo wa kitaifa wa ulinganifu wa sifa na tuzo katika ngazi zote.*

**(d) Suala: Elimu ya lazima na muda wa elimu na mafunzo**

**Maelezo**

Muundo wa elimu na mafunzo uliopo unatoa fursa ya mtoto kujiunga na elimu ya awali kwa muda wa miaka miwili. Hata hivyo, uchambuzi unaonesha kuwa mtaala unaotumika unaweza kufundishwa kwa mwaka mmoja kama ukifundishwa kwa ufanisi. Pia, Itifaki ya Dakar ya mwaka 2000 ambayo Tanzania imeiridhia, na kwa mujibu wa UNESCO (ISCED (International Standard Classification of Education), 2011) elimu ya awali inatakiwa kutolewa kwa watoto wenye umri kati ya miaka mitatu hadi sita. Pamoja na kutambua umuhimu wa elimu katika ngazi hii, Itifaki ya UNESCO inayataka mataifa kushiriki ili mtoto wa rika lengwa apate elimu katika ngazi husika kulingana na mazingira ya kila nchi.

Kwa sasa mazingira ya elimu ya awali nchini hayaridhishi kwa sababu ya ukosefu wa walimu wenye sifa, na miundombinu stahiki. Kwa mfano, wastani wa uwiano wa mwalimu na mwanafunzi ulikuwa 1:94 kwa mwaka 2022, wakati unaotakiwa ni 1:25. Darasa la elimu ya awali kwa sasa lina wastani wa wanafunzi 80 wakati kiwango cha wastani wa wanafunzi

RASIMU

kinachotakiwa ni 25.

Kwa sasa, elimu ya msingi inatolewa kwa miaka saba (7) na ni ya lazima kwa uandikishaji na mahudhurio kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Sura ya 353. Wahitimu wengi wa elimu ya msingi katika mfumo wa sasa wanakuwa na umri wa miaka 13. Baadhi ya wahitimu huendelea na elimu ya sekondari na mafunzo ya ufundi; waliokosa fursa hizo huingia kwenye ulimwengu wa kazi. Wahitimu hawa wanakuwa na umri mdogo na hawana maarifa na ujuzi unaotosheleza kujiunga na ulimwengu wa kazi au kukabiliana na changamoto za maisha iwapo watakosa fursa ya kuendelea na elimu ya sekondari ngazi ya chini au elimu ya ufundi.

Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani umeweka umri wa chini wa kuajiriwa katika baadhi ya kazi kuwa miaka 15. Kadhalika, Itifaki ya SADC (1997) kuhusu elimu na mafunzo inasisitiza kutokomeza kutojua kusoma na kuandika kwa kuweka juhudi ya kuwa na elimu ya lazima kwa wote kwa kipindi kisichopungua miaka tisa.

Kutokana na changamoto za muundo uliopo wa 2+7+4+2+3+ na makubaliano hayo, kuna umuhimu wa kurekebisha muundo wa elimu ya awali na msingi ya sasa ili elimu ya awali itolewe kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja kulingana na mahitaji ya mwanafunzi husika. Aidha, kila mtoto mwenye umri wa miaka 6 na ambaye amepata au hakupata elimu ya awali, kwa mujibu wa sheria, apatiwe elimu ya lazima itakayotolewa kwa muda wa miaka 10 ili kumwezesha mwanafunzi kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, kuwa na ufahamu wa jumla na pia kupata umahiri ikiwemo maarifa na ujuzi kulingana na

matakwa ya ngazi hiyo

**Madhumuni**

Kuwa na muda wa utoaji wa elimu na mafunzo wenye kuleta tija, ufanisi na matumizi bora ya rasilimali.

## MATAMKO

*3.1.14 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea na utaratibu wa utoaji wa elimu ya awali ya mwaka mmoja kwa watoto wenye umri wa miaka mitano kwa kuzingatia mahitaji yao, mazingira na hali halisi ya upatikanaji wa rasilimali nchini.*

*3.1.15 Serikali itaweka utaratibu wa elimu ya msingi na sekondari ngazi ya chini kuwa ya lazima na kutolewa kwa miaka kumi na umri wa kuanza darasa la kwanza kuwa miaka sita.*

*3.1.16 Serikali itaweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa muda wa kukamilisha elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali unalenga mwanafunzi kupata ujuzi na maarifa stahiki kwa kuzingatia Mfumo wa Tuzo wa Taifa.*

*3.1.17 Serikali itahakikisha kuwa elimu ya msingi na sekondari katika mfumo wa umma inatolewa bila ada.*

### 3.2 Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo

### (a) Suala: Fursa kwa usawa katika elimu na mafunzo

RASIMU

**Maelezo**

Ni muhimu kwa kila Mtanzania kupata fursa za elimu na mafunzo bila ubaguzi wa jinsi, rangi, kabila, dini, ulemavu na hali ya kijamii au kipato. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kupanua na kuboresha mazingira ya utoaji elimu jumuishi ili kila Mtanzania apate fursa za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji yake, mazingira na hali halisi ya upatikanaji rasilimali nchini.

Pamoja na juhudi za Serikali na wadau wengine, baadhi ya makundi bado hayajafikiwa kikamilifu kutokana na sababu za kijamii, kiuchumi na kijiografia, zikiwemo umbali wa kutembea kwenda shule, ajira za watoto, utoro, umaskini, ujauzito na ndoa za ututoni. Ili kufikia lengo la kutoa elimu kwa wote, kuna umuhimu wa kuondoa vikwazo vyote vinavyosababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kujiunga na kukamilisha mzunguko wa elimu.

**Madhumuni**

Watoto wote wa rika lengwa kujiunga na kukamilisha mzunguko wa elimu na mafunzo katika ngazi husika.

## MATAMKO

*3.2.1 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuongeza na kuimarisha kwa usawa fursa anuwai za elimu na mafunzo kwa makundi yote ya kijamii.*

*3.2.2 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaondoa vikwazo vinavyozuia wanafunzi wote kuendelea na masomo na*

*kukamilisha mzunguko wa elimu katika ngazi husika.*

*3.2.3 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuimarisha na kusimamia afua mbalimbali zinazolenga kutoa fursa za elimu kwa wale walioikosa.*

**(b) Suala: Usawa wa kijinsia katika elimu na mafunzo**

**Maelezo**

Ushiriki wa jinsi zote katika elimu na mafunzo ni muhimu ili kila Mtanzania ashiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeendelea kuhakikisha utoaji wa elimu na mafunzo unazingatia usawa wa kijinsia ili hata mmoja asiwachwe nyuma. Hata hivyo, ingawa uwiano wa kijinsi katika elimu ya msingi na sekondari ngazi ya chini unaridhisha, bado ushiriki wa wasichana katika elimu ya amali na elimu ya juu, hususan katika fani za sayansi, hisabati na teknolojia, hauridhishi. Hivyo, kuna umuhimu wa kuweka mazingira wezeshi kwa wasichana kushiriki katika elimu ya amali na elimu ya juu hususan katika fani tajwa.

**Madhumuni**

Kuwa na usawa wa kijinsia katika elimu na mafunzo.

## TAMKO

*3.2.4 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaweka mazingira wezeshi ya kuongeza ushiriki wa wasichana katika elimu ya amali na elimu ya juu hususan katika fani za sayansi, hisabati, na teknolojia.*

**(c) Suala: Elimu na mafunzo jumuishi katika ngazi zote**

**Maelezo**

Lengo la nne la Malengo ya Maendeleo Endelevu linahimiza uwepo wa mfumo jumuishi ambao haumnyimi mtoto yeyote haki ya kupata elimu. Katika mfumo huo, wanafunzi wote, wenye ulemavu na wasio na ulemavu, hujifunza pamoja kulingana na umri wao katika shule zilizopo katika jamii yao. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kuboresha mazingira ya kuwajumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kushiriki kikamilifu katika mfumo rasmi wa elimu.

Pamoja na juhudi hizo, bado kuna changamoto zinazoathiri utoaji wa elimu jumuishi ikiwemo ukosefu wa mfumo fanisi wa utambuzi wa watoto wenye mahitaji maalumu, uhaba mkubwa wa walimu mahiri wa elimu maalumu, uhaba wa vifaa saidizi na mtizamo hasi wa jamii kwa watoto wenye mahitaji maalumu. Hivyo, ni muhimu kuendelea kuboresha mfumo wa utoaji wa elimu na mafunzo katika mazingira jumuishi ili kutoa fursa kwa watoto wote kujifunza na kushirikiana.

**Madhumuni**

Kuwa na elimu na mafunzo jumuishi katika ngazi zote.

## MATAMKO

*3.2.5 Serikali itaimarisha mfumo wa utambuzi wa mahitaji maalumu ya kila mwanafunzi katika ngazi zote za elimu.*

*3.2.6 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha uwepo wa mazingira wezeshi ya utoaji wa elimu na mafunzo jumuishi katika ngazi zote.*

**(d) Suala: Utambuzi na uendelezaji wa vipaji na vipawa katika elimu na mafunzo**

**Maelezo**

Katika maendeleo ya Taifa, ni muhimu kutambua mapema na kuendeleza vipawa na vipaji katika fani mbalimbali kama sayansi na teknolojia, muziki, ngoma, sanaa, ufundi na michezo . Hata hivyo, utaratibu uliopo unazingatia ufaulu wa kitaaluma kama kigezo pekee cha kutambua vipaji na vipawa na hivyo kuwapoteza wanafunzi wengi wenye vipaji na vipawa katika maeneo mengine. Kuna umuhimu wa kutengeneza utaratibu utakaotambua wanafunzi wote wenye vipaji na vipawa kwa upana wake.

**Madhumuni**

Kuwa na mfumo fanisi wa elimu na mafunzo wa kubaini na kuendeleza vipaji na vipawa mbalimbali katika ngazi zote.

**Tamko**

*3.2.7 Serikali itaweka utaratibu wa kubaini na kuendeleza wanafunzi wenye vipaji na vipawa mbalimbali katika ngazi zote za elimu.*

**(e) Suala: Matumizi ya teknolojia katika elimu na mafunzo**

RASMI

**Maelezo**

Maendeleo ya teknolojia, hususan Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), yametoa fursa ya utoaji wa elimu na mafunzo kwa kutumia njia anuai zikiwemo za masafa, na hivyo kuwezesha mwalimu mmoja kuweza kufikia makundi mbalimbali ya wanafunzi kwa wakati mmoja. Katika mazingira kama ya kwetu, ambapo licha ya jitihada za Serikali, bado kuna uhaba wa walimu mahiri katika baadhi ya masomo kama ya lugha, hisabati na sayansi, njia hii inaweza kutumika kwa ufanisi kutoa elimu bora kwa wanafunzi wengi zaidi kwa kutumia idadi ndogo ya walimu mahiri, ikiwa miundombinu na vifaa vya TEHAMA kwa wanafunzi vitaongezeka.

**Madhumuni**

Kutumia teknolojia kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu na mafunzo.

**Matamko**

*3.2.8 Serikali itaweka utaratibu wa kutumia teknolojia ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*3.2.9 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha uwepo wa mazingira wezeshi ya utoaji wa elimu na mafunzo kwa kutumia teknolojia katika ngazi zote.*

**(f) Suala: Utambuzi wa watu waliopata ujuzi na maarifa nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo.**

**Maelezo**

Elimu na mafunzo nje ya mfumo rasmi ni njia mojawapo ya kujenga umahiri katika fani na stadi mbalimbali duniani kote. Serikali imeweka utaratibu wa kutambua na kurasimisha ujuzi unaopatikana nje ya mfumo rasmi katika fani mbalimbali za amali kwa lengo la kuwawezesha walengwa kushiriki kikamilifu katika ulimwengu wa kazi. Licha ya jitihada hizo, utaratibu uliopo sasa umejikita zaidi kwenye fani chache za kihandisi. Hivyo, kuna kila sababu za kuongeza wigo wa utaratibu huo ili uweze kujumuisha fani zote muhimu za amali.

**Madhumuni**

Kuwa na mfumo wa kutambua na kurasimisha ujuzi na stadi zinazopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo.

## TAMKO

*3.2.10 Serikali itaimarisha utaratibu wa utambuzi na urasimishaji wa ujuzi na stadi zinazopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo.*

### 3.3 Ubora wa Elimu na Mafunzo

Mfumo wa elimu unalenga kutoa elimu na mafunzo yanayotambulika kikanda na kimataifa na inayokidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa. Hoja hii imejikita katika masuala yafuatayo:

RASIMU

## (a) Suala: Uthibiti ubora wa elimu na mafunzo

**Maelezo**

Ubora wa elimu na mafunzo unatokana na ubora wa mitaala iliyopo, umahiri wa watekelezaji wa mitaala hiyo, uongozi, usimamizi, mazingira ya kutolea elimu na mafunzo, tathmini na rasilimali zilizopo. Pamoja na maboresho mbalimbali yaliyofanyika, bado kuna changamoto katika suala la ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.

Pamoja na ufaulu katika mitihani ya darasa la saba na kidato cha nne kuongezeka kutoka asilimia 57.0 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 79.7 mwaka 2022 kwa upande wa elimu ya msingi; na asilimia 69.8 mwaka 2014 hadi asilimia 87.8 mwaka 2022 kwa elimu ya sekondari ya chini, bado kiwango cha maarifa na ujuzi wa wahitimu katika ngazi hizo ni kidogo ikilinganishwa na ngazi ya elimu waliyofikia. Kadhalika, maarifa na ujuzi wa wahitimu wa mafunzo ya ufundi na elimu ya juu hayakidhi mahitaji mbalimbali katika ulimwengu wa kazi.

Tathmini zinaonesha kwamba, ili kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo nchini, kuna ulazima wa kuwa na mitaala bora na uthibiti fanisi wa elimu; na piauimarishaji wa upimaji na tathmini, ithibati na mamlaka zinazohusika na masuala hayo.

Wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo ina jukumu la kufuatilia ubora wa elimu katika ngazi zote kwa kuzingatia mitaala na viwango vilivyowekwa. Uthibiti ubora wa elimu ya awali, elimu ya msingi, sekondari na elimu ya ualimu unaoratibiwa na Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule umekuwa ukikabiliwa na

RASMI

changamoto mbalimbali na hivyo kushindwa kufikia matarajio. Pamoja na kutumika kwa dhana ya uthibiti ubora wa shule yenye kuhitaji ushirikishwaji wa wadau na mbinu mbadala, changamoto iliyopo ni kuendelea kwa dhana ya ukaguzi wa shule wenye kujikita katika uhakiki wa orodha ya masuala yanayohitajika kufanyika katika ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo, bado kuna uhitaji wa kuimarisha utekelezaji wa dhana ya uthibiti ubora iliyokusudiwa yenye kuzingatia ushirikishwaji na uwajibikaji wa pamoja wa Kamati na Bodi za Shule na Vyuo, wakuu wa vyuo vya ualimu, walimu wakuu, wakuu wa shule, walimu, wakufunzi pamoja na wazazi katika suala la usimamizi na uthibiti wa ubora wa elimu itolewayo nchini.

Kwa upande mwingine, Wizara imekasimu jukumu la kuratibu ithibati na uthibiti ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (amali) kwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Aidha, Wizara imekasimu jukumu la kuratibu ithibati na uthibiti ubora wa elimu ya juu ya jumla kwa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Vyombo hivi vya ithibati vinashirikiana na taasisi nyingine wezeshi ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Elimu Tanzania, Baraza la Mitihani Tanzania, Bodi ya Huduma za Maktaba, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Mamlaka ya Elimu Tanzania katika kuinua ubora wa elimu. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto za kiutendaji na za kiuratibu zinazoathiri viwango vya ubora wa elimu katika ngazi mbalimbali.

Hivyo, uhusiano baina ya taasisi na wizara zenye jukumu la kuwezesha utoaji wa elimu na mafunzo nchini na Wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo unahitaji kufanyiwa tathmini ya mara kwa mara kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika, kwa lengo likiwa kuongeza tija. Sheria za taasisi hizo zinahitaji kutathminiwa ili kuleta ufungamano katika mfumo wa ithibati,

uthibiti, usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo nchini.

**Madhumuni**

Kuwa na ufanisi katika uratibu, usimamizi, ithibati na uthibiti katika utoaji wa elimu na mafunzo.

## MATAMKO

*3.3.1 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha mfumo, muundo na taratibu za usimamizi, ithibati na uthibiti ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*3.3.2 Serikali itaimarisha ithibati na uthibiti ubora wa elimu ya ualimu kwa kuweka utaratibu unaojumuisha ngazi mbalimbali za taaluma ya ualimu.*

*3.3.3 Serikali itahakikisha vyombo vya usimamizi, uendeshaji na wezeshi katika utoaji wa elimu na mafunzo vinahusiana kiutendaji katika ngazi zote.*

*3.3.4 Serikali itaimarisha mfumo, mbinu, dhana, na falsafa ya uthibiti ubora wa elimu na mafunzo ili kuleta ufanisi wa utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

**(b) Suala: Mitaala ya elimu na mafunzo**

**Maelezo**

Mtaala ni mwongozo wa elimu katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo ambao ikiwa hautaandaliwa vizuri,

RASIMU

kutekelezwa ipasavyo au kutathminiwa kwa umakini, mfumo wa elimu utashindwa kufanya kazi kwa tija na hautaweza kuleta matarajio yanayokusudiwa na jamii. Hadi mwaka 2005 mitaala iliyokuwepo kwa upande wa elimu ya awali, msingi, sekondari na elimu ya ualimu ilijikita zaidi katika maudhui ya ufahamu na kuwa na msisitizo mdogo katika kujenga ujuzi. Kuanzia mwaka 2005 mitaala hiyo iliboreshwa na kuwa ya kujenga umahiri, kwa kuingiza stadi za kuajirika kutokana na mfumo wa kutoa mafunzo ya uwili (utoaji wa mafunzo kwa nadharia na vitendo) kwa kushirikiana na viwanda, mashamba, na taasisi za huduma ili kuunganisha utoaji wa mafunzo kwa nadharia na vitendo. Hata hivyo, hapakuwa na maandalizi ya kutosha ya utekelezaji wa mitaala hiyo, mathalan, maandalizi ya walimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kuna umuhimu wa kuimarisha mitaala katika ngazi zote pamoja na kuhakikisha kwamba walimu wanatayarishwa vyema kumudu kutekeleza mitaala ya kujenga umahiri.

Kuna hisia kwamba baadhi ya mitaala ya amali na elimu ya juu haiwaandai ipasavyo wahitimu wake kwa ulimwengu wa kazi. Kuna umuhimu wa kupitia upya mitaala ya elimu ya amali na elimu ya juu ili ikidhi mahitaji ya ulimwengu wa kazi. Tathmini pia zinaonesha kuwa kuna tofauti kubwa ya maudhui katika baadhi ya programu za elimu ya juu ambazo kimsingi zingetakiwa kufanana. Kwa mantiki hiyo, kuna umuhimu wa kuweka vigezo vya ulinganifu (benchmarks) baina ya programu zinazofanana katika taasisi mbalimbali. Aidha, upo umuhimu wa mitaala ya ngazi zote kuzingatia stadi za msingi za Karne ya 21 kama vile kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi, utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijitali, maadili na uzalendo.

**Madhumuni**

Kuwa na mitaala yenye tija na fanisi na inayokidhi mahitaji ya ulimwengu wa kazi katika kuleta maendeleo ya Taifa na kuhimili ushindani.

## MATAMKO

*3.3.5 Serikali itahakikisha uwepo wa mitaala bora katika ngazi zote za elimu na mafunzo inayoendana na wakati na inayozingatia mahitaji ya Taifa na ulimwengu wa kazi.*

*3.3.6 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha mitaala inalenga kukuza Stadi za Karne ya 21 ambazo ni kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi, utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijitali, maadili na uzalendo, katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*3.3.7 Serikali itahakikisha kuwa mitaala ya elimu ya ualimu inawaandaa walimu kutekeleza kwa ufanisi mitaala ya ujenzi wa umahiri na kukuza Stadi za Karne ya 21 kwa wanafunzi.*

*3.3.8 Serikali itahakikisha kuwa mafunzo ya ualimu yanakuwa na mwendelezo wa kitaaluma na kitaalamu kati ya ngazi moja na nyingine.*

*3.3.9 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha utoaji wa elimu ili kuwezesha wahitimu wa ngazi zote kupata maarifa na ujuzi wa kuchangia kikamilifu katika maendeleo yao, ya jamii na taifa.*

RASMI

*3.3.10 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha utaratibu wa uwili katika utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote kwa ushirikiano na viwanda, mashamba na sekta nyingine za uzalishaji na utoaji huduma.*

*3.3.11 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itazingatia utekelezaji wa mitaala inayoakisi mahitaji ya ujuzi kulingana na mazingira na rasilimali zilizopo katika maeneo husika.*

*3.3.12 Serikali itaimarisha usimamiaji na upimaji wa utekelezaji wa mitaala katika taasisi za elimu na mafunzo katika ngazi zote, ili kuleta ufanisi wa elimu na mafunzo yatolewayo.*

**(c) Suala: Elimu ya sayansi na teknolojia**

**Maelezo**

Elimu ya sayansi na teknolojia ni muhimu katika kumwezesha mwananchi kumudu mazingira yake na kuchangia katika maendeleo ya Taifa. Watoto huanza kufundishwa somo la sayansi Darasa la III na katika elimu ya sekondari ngazi ya chini, wanafunzi wote husoma Fizikia, Kemia, Baiolojia na Hisabati hadi kidato cha pili (2). Aidha, wanafunzi wote huendelea kusoma Baiolojia na Hisabati hadi kidato cha nne (4). Baadhi ya wanafunzi huchagua kuendelea na masomo ya Fizikia na Kemia kuanzia kidato cha tatu (3) hadi cha nne (4). Takwimu zinaonesha kuwa ni asilimia 30-35 tu ya ya wanafunzi wanasoma masomo ya sayansi katika kidato cha tatu (3) na cha nne (4). Hao wakifaulu ndiyo wanatarajiwa kusomea fani mbalimbali za sayansi na teknolojia katika vyuo vya elimu ya juu na vyuo vya elimu ya ufundi sanifu na mafunzo ya ufundi stadi.

RASIMU

Mitaala ya elimu ya msingi na sekondari inatakiwa kuweka mkazo katika elimu ya sayansi na teknolojia. Makubaliano kuhusu Elimu ya Sayansi na Teknolojia (UNESCO-PERTH 2007) yanasisitiza kufanya mapitio ya mitaala ya elimu ya sayansi na teknolojia ili kuongeza hamasa ya wanafunzi kutambua umuhimu wa sayansi na teknolojia katika jamii. Pia kuna umuhimu wa kuweka mkazo katika matumizi ya sayansi na teknolojia katika kufundisha na kujifunza.

TEHAMA ni nyenzo muhimu katika ulimwengu wa kazi. Endapo TEHAMA itafundishwa kwa ufanisi itawezesha kujenga rasilimaliwatu yenye ujuzi stahiki kwa maendeleo ya taifa. Tanzania ni moja ya nchi duniani zenye kiwango cha chini cha ufundishaji wa/kwa TEHAMA katika elimu na mafunzo. Aidha, kuna upungufu wa vifaa na rasilimaliwatu katika ufundishaji wa TEHAMA. Upungufu huo unasababisha wahitimu kukosa umahiri stahiki wa kuchagiza maendeleo ya sayansi na teknolojia na kuiwezesha nchi kujenga uchumi shindani katika dunia ya utandawazi. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Hisabati, Sayansi na Teknolojia, hususan TEHAMA, katika ngazi zote za elimu na mafunzo. Aidha, kuimarisha ufundishaji wa masomo hayo ni moja ya nyenzo muhimu ya kukuza ubunifu na uwezo wa kutatua matatizo.

**Madhumuni**

Kuongeza idadi ya wananchi walioelimika katika sayansi na teknolojia na wanaomudu kuitumia katika kuboresha maisha yao ya kila siku.

## MATAMKO

*3.3.13 Serikali itaimarisha muundo na utaratibu wa ufundishaji wa Hisabati, Sayansi na Teknolojia katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*3.3.14 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuhamasisha ujifunzaji wa Hisabati, Sayansi, na Teknolojia katika ngazi zote za elimu na mafunzo na katika jamii.*

*3.3.15 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Hisabati, Sayansi na Teknolojia, ikiwemo TEHAMA, katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

**(d) Suala: Nyenzo, vifaa, zana na mbinu za kufundishia na kujifunzia**

**Maelezo**

Utekelezaji fanisi wa mitaala unategemea upatikanaji wa nyenzo, vifaa na zana stahiki za kufundishia na kujifunzia, kulingana na mahitaji ya masomo na programu katika ngazi mbalimbali za elimu. Nyenzo, vifaa, na zana hizo ni pamoja na vitabu vya kiada na ziada, kemikali za maabara, mitambo na karakana. Kumekuwa na upungufu wa nyenzo, vifaa na zana bora za kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu. Vilevile, mfumo wa uandaaji, uchapishaji na usambazaji wa vitabu na uandaaji wa zana na nyenzo nyingine, bado una changamoto. Aidha, baadhi ya vifaa, zana na nyenzo zilizopo, ama zimepitwa na wakati au haziendani na mahitaji ya sasa. Hali hii imekuwa ikichangia kudhoofisha utoaji wa elimu.

Katika hali hii, kuna kila sababu ya kuendelea kuboresha utaratibu wa upatikanaji wa vitabu, nyenzo, vifaa na zana bora na za kutosha zinazokidhi mahitaji. Vilevile, ni muhimu kuwa na mfumo wenye tija wa uandaaji, uchapishaji na usambazaji wa vifaa vyote vya kufundishia na kujifunzia. Aidha, ni hitaji la msingi kutenga rasilimalifedha za kutosha kukidhi mahitaji ya wanafunzi kulingana na viwango vilivyowekwa. Ni muhimu pia kuhamasisha utamaduni wa kujisomea na kuimarisha huduma za maktaba na njia mbadala za upatikanaji wa maarifa.

**Madhumuni**

Kuwa na mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia.

## MATAMKO

*3.3.16 Serikali itahakikisha uwepo wa vifaa, nyenzo na zana stahiki za kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*3.3.17 Serikali itatoa na kusimamia matumizi ya kitabu kimoja cha kiada kwa kila somo kwa kila mwanafunzi katika elimu ya msingi na sekondari.*

*3.3.18 Serikali itahakikisha uwepo wa mfumo wenye tija wa uandaaji, uchapishaji na usambazaji wa vifaa vyote vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu.*

*3.3.19 Serikali itasimamia upatikanaji na matumizi ya vitabu vya ziada na rejea kwa kila somo katika elimu ya msingi na sekondari ambavyo vitaidhinishwa kwa utaratibu maalumu.*

RASIMU

*3.3.20 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha uwepo wa rasilimalifedha za kutosha kukidhi mahitaji ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kulingana na viwango vilivyowekwa katika ngazi zote za elimu.*

*3.3.21 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha huduma za maktaba na njia mbadala za upatikanaji wa maarifa katika shule, vyuo na jamii ili kuhamasisha utamaduni wa kujisomea.*

**(e) Suala: Miundombinu katika taasisi za elimu na mafunzo**

**Maelezo**

Ufanisi katika utoaji elimu unategemea kwa kiwango kikubwa uwepo wa miundombinu bora. Katika miaka ya hivi karibuni, Serikali imeongeza miundombinu pamoja na samani katika taasisi zote za elimu. Pamoja na jitihada za Serikali kuboresha miundombinu, bado kuna umuhimu wa kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa samani katika taasisi zake ili kufikia viwango vya ubora stahiki.

**Madhumuni**

Kuwa na miundombinu na samani toshelevu katika taasisi za elimu na mafunzo.

## TAMKO

RASIMU

*3.3.22 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha uwepo wa miundombinu bora na toshelevu katika taasisi za elimu na mafunzo.*

**(f) Suala: Mazingira salama na rafiki na huduma muhimu katika taasisi za elimu**

**Maelezo**

Mazingira salama na rafiki pamoja na huduma muhimu ni mahitaji ya msingi katika kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa kuna mazingira salama na rafiki katika taasisi za elimu. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya taasisi ambazo zinakabiliwa na mazingira yasiyoridhisha kwa utoaji wa elimu stahiki.

Vilevile, Serikali imehakikisha uwepo wa huduma muhimu, zikiwa ni pamoja na chakula, maji safi na salama, vituo vya afya, umeme, mawasiliano na usafiri katika taasisi za elimu. Pamoja na jitihada hizo, bado kuna changamoto katika upatikanaji wa huduma bora na muhimu. Hivyo, kuna umuhimu wa kuendelea kuboresha mazingira na huduma zinazokidhi mahitaji muhimu ya utoaji bora wa elimu na mafunzo katika taasisi zote.

**Madhumuni**

Kuwa na mazingira salama na rafiki na huduma muhimu katika taasisi za elimu na mafunzo.

**Matamko**

*3.3.23 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha uwepo*

*wa mazingira salama na rafiki katika taasisi za elimu na mafunzo. ###*

*3.3.24 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha kuwa huduma muhimu zikiwemo chakula, mawasiliano, umeme, maji safi na salama na afya zinapatikana katika taasisi za elimu na mafunzo.*

**(g) Suala: Ushauri na unasihi katika elimu na mafunzo**

**Maelezo**

Afya ya akili na mtizamo chanya ni mahitaji ya msingi katika kuhakikisha tija katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kuwezesha upatikanaji wa huduma za ushauri na unasihi ili kuimarisha afya ya akili na mtizamo chanya kwa walimu na wanafunzi kwa lengo la kujenga mwelekeo, tabia na kuendeleza mila, desturi na maadili mema katika jamii. Pamoja na jitihada hizo za Serikali, bado kuna changamoto ya utoshelevu na ufanisi katika utoaji wa huduma hizo katika taasisi za elimu na mafunzo, hususan katika shule za msingi na sekondari, na hivyo kuchangia mmomonyoko wa maadili, ikiwemo mimba za utotoni, utoro, na utovu wa nidhamu. Hali hii huchangia pia katika msongo wa mawazo na sonono, na uchaguzi wa masomo usio sahihi. Hivyo, ni muhimu kuimarisha utoaji wa huduma za ushauri na unasihi kwa wanafunzi na wafanyakazi katika taasisi zote za elimu na mafunzo.

**Madhumuni**

Kuwa na huduma ya ushauri na unasihi inayokidhi mahitaji kwa wanafunzi na wafanyakazi katika taasisi za elimu na mafunzo.

## TAMKO

*3.3.25 Serikali itaimarisha utoaji wa huduma stahiki ya ushauri na unasihi katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

### (h) Suala: Elimu yenye kudumisha uzalendo na amani

**Maelezo**

Utandawazi, tofauti za kiuchumi na mwingiliano wa watu wenye tamaduni mbalimbali umechangia katika kuleta mabadiliko ya maadili na tabia na hivyo kuleta changamoto mbalimbali katika jamii. Elimu katika taifa ni mhimili wa kudumisha amani ya jamii kwa kujenga stadi za kutatua migogoro, kujenga umoja wa kijamii na mshikamano. Kuna umuhimu wa kuwa na elimu itakayolenga kuwasaidia wanafunzi kujenga uwezo wa kuzuia na kutatua migogoro kwa amani inapotokea miongoni mwa watu na baina ya makundi, kitaifa au kimataifa. Hivyo, mitaala ya elimu na mafunzo iandaliwe kumwezesha Mtanzania kuelewa, kulinda na kuendeleza misingi ya maadili ya Taifa na uadilifu ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji, pamoja na kuthamini haki za kiraia na wajibu na majukumu yake.

**Madhumuni**

Kuwa na mhitimu mzalendo na mwenye kudumisha amani katika jamii.

## TAMKO



RASMI

*3.3.26 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha stadi za kudumisha amani, uzalendo na maadili zinajumuishwa katika mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*3.3.27 Serikali itaweka utaratibu wa kuhakikisha historia ya Tanzania inafundishwa katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

**(i) Suala: Matumizi ya Kiswahili, Kiingereza, lugha nyingine za kigeni na Lugha ya Alama ya Tanzania katika mawasiliano.**

**Maelezo**

Ubora wa elimu na mafunzo kwa kiasi kikubwa unategemea uelewa wa lugha kwa walimu na wanafunzi katika kufikisha na kupokea maarifa. Lugha za Kiswahili na Kiingereza, na lugha nyingine za kigeni zinafundishwa kama masomo katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Aidha, Lugha ya Alama ya Tanzania na maandishi ya Breli ni masomo yanayofundishwa katika vyuo vya ualimu.

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Taifa na inatumika kama lugha ya kwanza au ya pili miongoni mwa wananchi wengi. Kiswahili kimekuwa kwa kiwango cha kimataifa ambapo kinatumiwa na wengi kupata maarifa na ujuzi katika njanja mbalimbali. Aidha, Tanzania imeridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa kuhusiana na maendeleo na matumizi ya Kiswahili, na Tanzania imechaguliwa kuwa makao makuu ya Taasisi ya Kuendeleza Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Lugha ya Kiingereza inatumika kama lugha ya pili au ya tatu kwa baadhi ya wananchi. Kiswahili na Kiingereza ni lugha rasmi za kiofisi. Ufahamu mzuri wa lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kigeni pia unamwezesha Mtanzania kuwasiliana na watu wa mataifa mengine na kupata elimu, ujuzi na maarifa. Aidha, lugha za alama na maandishi ya Breli hutumika kwa mawasiliano baina ya viziwi, wasioona, viziwi wasioona, uoni hafifu, na watu wengine.

Kwa kutambua umuhimu wa lugha, Serikali imeendelea kuboresha ufundishaji wa masomo ya lugha katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Pamoja na juhudi hizo, bado kuna changamoto ya mawasiliano inayotokana na uelewa mdogo wa lugha. Sehemu kubwa ya changamoto hizo inatokana na mbinu duni, miundombinu na vifaa hafifu vya kufundishia na kujifunzia, ukosefu wa walimu mahiri wa lugha, na matumizi madogo ya lugha za kigeni katika mazingira ya kawaida. Kwa kuzingatia changamoto hizo, ni muhimu kuendelea kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, Kiingereza, lugha nyingine za kigeni, LAT na maandishi ya Breli.

**Madhumuni**

Kuwa na uwezo wa kutumia lugha mbalimbali katika mawasiliano.

## MATAMKO

*3.3.28 Serikali itahakikisha kuwa lugha ya Kiswahili, Kiingereza na nyingine za kigeni zinafundishwa kwa ufasaha na ufanisi katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*3.3.29 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itawezesha na kuendeleza Lugha ya Alama ya Tanzania na maandishi ya Breli kutumika katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

### (j) Suala: Lugha ya kufundishia

**Maelezo**

Lugha ya kufundishia ikitumika ipasavyo ina athari chanya katika matokeo ya ujifunzaji. Kwa sasa, lugha za kufundishia ni Kiswahili na Kiingereza. Lugha ya kufundishia elimu ya awali na msingi ni Kiswahili. Aidha, Lugha ya Kiingereza inatumika kufundishia katika baadhi ya shule za msingi kwa utaratibu maalumu. Vilevile, Lugha ya Kiingereza hutumika kufundishia katika shule za sekondari, vyuo vya ualimu ngazi ya stashahada, vyuo vya ufundi na vyuo vya elimu ya juu. Lugha ya Kiswahili hutumika kufundishia katika vyuo vya ualimu ngazi ya cheti, vyuo vya ufundi stadi na baadhi ya shule za sekondari inapohitajika.

Uzoefu wa nchi nyingine umeonesha umuhimu wa kutumia lugha inayotumiwa na wengi katika kujenga utambulisho na utamaduni wa nchi husika. Kwa hivyo, upo umuhimu wa kusisitiza matumizi ya Kiswahili katika kufundishia masomo yanayojenga uelewa wa utamaduni na Historia ya Mtanzania ili kuihifadhi na kuitangaza. Aidha, lugha ya Kiingereza ni nyenzo muhimu ya kuwezesha kupata maarifa. Hivyo, ni muhimu kutumia lugha ya Kiswahili ambayo inaeleweka na wengi na lugha ya Kiingereza ambayo ni chanzo kikuu cha maarifa katika kufundishia.

**Madhumuni**

Kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika ufundishaji.

## MATAMKO

*3.3.30 Lugha ya Taifa ya Kiswahili itatumika kufundishia katika elimu ya awali na elimu ya msingi, isipokuwa masomo ya lugha za kigeni na katika shule zitakazoomba kutumia lugha ya Kiingereza kufundishia.*

*3.3.31 Lugha ya Kiingereza itatumika kufundishia kuanzia ngazi ya sekondari ya chini, isipokuwa somo la Kiswahili, masomo ya lugha za kigeni na katika shule za sekondari na vyuo vitakavyoruhusiwa kutumia Lugha ya Kiswahili kufundishia.*

*3.3.32 Lugha ya Taifa ya Kiswahili itatumika kufundishia Somo la Historia ya Tanzania na Maadili ili kujenga na kuendeleza mila, desturi na utamaduni wa Mtanzania katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

**(k) Suala: Upimaji na tathmini ya maendeleo ya wanafunzi katika elimu na mafunzo**.

**Maelezo**

Upimaji na tathmini ni muhimu katika kubaini maendeleo ya mwanafunzi na changamoto anazozikabili katika ujifunzaji. Aidha, upimaji unampa mwalimu fursa ya kutathmini tija katika ufundishaji na kufanya maboresho stahiki. Utaratibu wa sasa wa upimaji unazingatia upimaji endelevu na upimaji tamati katika ngazi zote za elimu. Hata hivyo, baada ya kuanzisha mitaala inayosisitiza ujenzi wa umahiri, utaratibu wa upimaji haukubadilishwa kuendana na mabadiliko hayo. Vilevile, hakuna msisitizo kwenye ujenzi wa

Stadi za Karne ya 21 kama ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo.

Hivyo basi, ni muhimu kuboresha mfumo wa upimaji kwa kutumia vigezo vinavyotambuliwa vya upimaji wa maendeleo ya kila siku ya mwanafunzi na tathmini ya mwisho ya kukamilisha ngazi husika kwa kuzingatia mtaala wa ujenzi wa umahiri na kukuza Stadi za Karne ya 21.

**Madhumuni**

Kuwa na upimaji na tathmini fanisi wa maendeleo ya mwanafunzi.

## TAMKO

*3.3.33 Serikali itaweka mfumo wa upimaji endelevu na tamati utakaozingatia mtaala wa ujenzi wa umahiri na kukuza Stadi za Karne ya 21 katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

### 3.4 Rasilimaliwatu

**(c) Suala: Upatikanaji wa walimu, wakufunzi, na wahadhiri mahiri kwa ajili ya sekta ya elimu**

**Maelezo**

Uwepo wa rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha ikiwemo walimu, wakufunzi na wahadhiri ni msingi wa utoaji wa elimu bora katika ngazi zote. Serikali imeendelea kuongeza idadi na ubora wa

RASIMU

rasilimaliwatu katika sekta ya elimu. Hata hivyo, uhitaji wa rasilimali hizo katika shule za awali hadi sekondari umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka hususan katika masomo ya sayansi, lugha, hisabati na fani za amali. Aidha, kuna upungufu mkubwa wa wakufunzi na wahadhiri katika taasisi za elimu ya amali na elimu ya juu.

Kuna umuhimu wa kuwa na mfumo wa kutambua mahitaji ya rasilimaliwatu katika kila ngazi ya elimu na mafunzo, na kuiandaa kulingana na vipaumbele vya Taifa. Aidha, kuna umuhimu wa kuimarisha taratibu za ajira na mgawanyo wa rasilimaliwatu ili kukidhi mahitaji halisi katika kila taasisi na katika ngazi zote za elimu.

Vilevile, kuna umuhimu wa kuweka mazingira bora yatakayohakikisha kwamba vijana wengi mahiri wanajiunga na kubaki katika fani ya ualimu hususan katika masomo ya sayansi, hisabati, lugha na elimu ya amali. Upo umuhimu pia wa kuwavutia na kuwabakiza wahadhiri kazini ili kuinua ubora wa elimu, utafiti, na huduma za jamii katika taasisi za elimu ya juu.

**Madhumuni**

Kuwa na rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha katika ngazi zote za elimu.

## MATAMKO

*3.4.1 Serikali itaweka utaratibu wa kutambua mahitaji na vipaumbele vya Taifa ili kuandaa walimu, wakufunzi na wahadhiri kulingana na vipaumbele katika ngazi zote.*

*3.4.2 Serikali itaweka mfumo fanisi wa mgawanyo wa walimu, wakufunzi na wahadhiri unaozingatia uhitaji katika kila eneo na kila ngazi.*

*3.4.3 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaweka mfumo fanisi wa kuwavutia na kuwabakiza walimu, wakufunzi na wahadhiri kwa kuboresha maslahi yao na mazingira ya kazi katika ngazi zote.*

*3.4.4 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaweka mfumo fanisi wa kuwavutia na kuwabakiza walimu, wakufunzi na wahadhiri wanaofanya kazi katika mazingira magumu ikiwemo maeneo ya pembezoni katika ngazi zote.*

*3.4.5 Serikali itaweka utaratibu wa utambuzi na usajili wa walimu na wakufunzi ili kuongeza hadhi na fursa za ajira.*

*3.4.6 Serikali itaimarisha mfumo wa ajira ya walimu, wakufunzi, na wahadhiri kwa kuhakikisha kuwa wenye sifa na viwango stahiki wanaajiriwa baada ya kufanya mitihani na kufaulu kama sehemu ya usaili.*

*3.4.7 Serikali itaweka utaratibu wa kuwaandaa na kuwaendeleza wahadhiri kitaaluma kufikia viwango vyenye hadhi ya kimatatifa.*

*3.4.8 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha mfumo wa utoaji wa mafunzo kazini kwa walimu, wakufunzi na wahadhiri kwa kuzingatia dhana ya elimu bila ukomo.*

*3.4.9 Serikali itaweka utaratibu wa kuongeza ushindani wa taasisi za elimu ya juu kwa kuwavutia na kuwabakiza wahadhiri*

RASIMU

*wenye hadhi ya kimatatifa kwa kuzingatia uwezo wao katika utafiti, machapisho na huduma za kitaalamu.*

**(d) Suala: Upatikanaji wa rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha kwa maendeleo ya taifa**

**Maelezo**

Uwepo wa rasilimaliwatu mahiri na katika uwiano wa kutosha katika sekta zote za uchumi ni muhimu kwa maendeleo ya kitaifa. Serikali imeendelea kuongeza idadi na ubora wa rasilimaliwatu katika sekta zote kufikia kiwango cha kuridhisha. Kwa miaka ya hivi karibuni, Taifa limeweka mkazo katika upanuzi wa elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu na hivyo kusababisha uwepo wa ombwe la rasilimaliwatu katika kada ya kati, hususan wenye elimu ya amali. Tatizo hilo lilikuzwa na utaratibu wa kubadilisha baadhi ya taasisi za elimu ya kati kuwa vyuo vya elimu ya juu. Kuna umuhimu wa kujenga uwiano stahiki wa rasilimaliwatu yenye ujuzi katika fani mbalimbali, hususan zile za vipaumbele vya Taifa.

**Madhumuni**

Kuwa na rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali kwa maendeleo ya Taifa.

## MATAMKO

*3.4.10 Serikali itaweka utaratibu wa kufanya tathmini ya mara kwa mara ili kujua mahitaji halisi ya rasilimaliwatu katika kila ngazi.*

*3.4.11 Serikali itaweka mazingira wezeshi kwa sekta ya elimu na*

*mafunzo kuandaa rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha kulingana na mahitaji ya Taifa.*

## 3.5 Usimamizi na Uendeshaji Madhubuti wa Elimu na Mafunzo

### (f) Suala: Uongozi, usimamizi na uendeshaji fanisi katika sekta ya elimu

**Maelezo**

Uongozi na usimamizi madhubuti wa sekta ya elimu ni muhimu ili kuleta tija na ufanisi katika utoaji wa elimu na mafunzo. Serikali imeendelea kuimarisha uongozi na usimamizi katika sekta ya elimu ikiwemo kuanzishwa na kuendelezwa kwa Wakala wa Uongozi wa Maendeleo ya Elimu. Vilevile, Serikali imekuwa ikifanya mabadiliko ya viongozi pale inapoona inafaa ili kuimarisha uongozi, usimamizi na kuongeza tija katika sekta ya elimu.

Hata hivyo, bado kuna changamoto katika usimamizi na uendeshaji wa sekta ya elimu ikiwemo kufanyika kwa mabadiliko yasiyozingatia kikamilifu mahitaji na ushirikishwaji wa jamii. Aidha, bado kuna mgongano wa baadhi ya sheria, taratibu, kanuni na miongozo inayosimamia uendeshaji na utoaji wa elimu na mafunzo. Kwa upande wa uendeshaji, baadhi ya wadau wameonyesha wasiwasi kuhusu utendaji wa baadhi ya viongozi katika sekta ya elimu. Hii inaweza kuashiria upungufu katika sifa na uwezo wao kama viongozi. Kutokana na changamoto hizo, kuna umuhimu wa kuhuisha sheria, taratibu, kanuni na miongozo inayohusu uendeshaji na usimamizi wa elimu na mafunzo. Vilevile, kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa mabadiliko yote makubwa katika sekta ya elimu yanatokana na tafiti za kisayansi na

ushirikishwaji wa jamii. Aidha, kuna umuhimu wa kuimarisha utaratibu wa kuwapata viongozi katika sekta ya elimu, na kuhakikisha kuwa utaratibu huo unafuatwa.

**Madhumuni**

Kuwa na uongozi, usimamizi na uendeshaji wenye tija na uwajibikaji katika sekta ya elimu.

## MATAMKO

*3.5.1 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha mabadiliko ya kimkakati katika sekta ya elimu yanazingatia sheria, matokeo ya tafiti, mahitaji na ushirikishwaji wa wadau muhimu.*

*3.5.2 Serikali itahuisha sheria, taratibu, kanuni na miongozo, pamoja na muundo wa uongozi na usimamizi, ili kuwa na mfumo wa uendeshaji wa sekta ya elimu wenye tija.*

*3.5.3 Serikali itaimarisha utaratibu wa kuwapata viongozi bora katika nafasi za usimamizi wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*3.5.4 Serikali itahakikisha kwamba sheria za taasisi za elimu ya juu zinatekelezwa kikamilifu kwa kuzingatia majukumu yao ya msingi.*

**(g) Suala: Ushirikiano katika elimu na mafunzo kati ya Tanzania Bara na Zanzibar**

**Maelezo**

RASIMU

Ushirikiano madhubuti katika masuala kati ya Tanzania Bara na Zanzibar ni muhimu ili kuleta tija na ufanisi katika utoaji wa elimu na mafunzo. Kikatiba, elimu ya msingi, sekondari, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi sio masuala ya Muungano. Elimu ya juu ni suala la Muungano. Hata hivyo, kuna ushirikiano wa karibu katika utekelezaji wa masuala mbalimbali ya elimu ikiwemo mitaala na upimaji kwa ngazi ya sekondari na elimu ya ufundi. Kwa kuzingatia hayo, kuna umuhimu wa kuendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar katika utoaji wa elimu na mafunzo kwa ngazi zote ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu ya juu.

**Madhumuni**

Kuwa na ushirikiano na uhusiano thabiti katika masuala ya elimu na mafunzo kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.

**Tamko**

*3.5.5 Serikali itaendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano katika elimu na mafunzo kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.*

**(h) Suala: Ushirikiano katika elimu na mafunzo kikanda na kimataifa**

**Maelezo**

Mwingiliano wa kiuchumi, kisiasa na kijamii baina ya Tanzania, nchi marafiki na jumuiya za kikanda na kimataifa unatutaka kuhakikisha kuwa na elimu na mafunzo yenye ubora na shindani. Pamoja na Tanzania kuridhia mikataba, itifaki na makubaliano

mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo imechangia kuinua ubora wa elimu na mafunzo, bado zipo changamoto za kisera, kisheria, kimfumo, kimuundo na kijamii zinazopaswa kutatuliwa kwa lengo la kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo. Changamoto hizo zimesababisha baadhi ya itifaki, makubaliano na mikataba kusitishwa au kutokutekelezwa kama ilivyokusudiwa. Hivyo, kuna umuhimu wa kutathmini na kuondoa vikwazo vinavyoathiri mahusiano ya kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo.

**Madhumuni**

Kuwa na uhusiano na ushirikiano wenye tija wa kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo.

## TAMKO

*3.5.6 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo.*

*3.5.7 Serikali itaendelea kutathmini na kuondoa vikwazo vinavyoathiri mahusiano na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo.*

**(i) Suala: Upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya maendeleo ya elimu na mafunzo**

**Maelezo**

Ardhi ni rasilimali muhimu kwa uanzishaji na upanuzi wa taasisi za elimu na mafunzo. Mahitaji ya ardhi ya taasisi za elimu na mafunzo yanaendelea kuongezeka kutokana na azma ya Serikali

RASIMU

kupanua fursa za elimu katika ngazi zote. Aidha, baadhi ya taasisi na asasi za elimu na mafunzo zimejengwa katika ardhi ambayo haziimiliki kisheria. Vilevile, kumekuwepo na uvamizi wa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya baadhi ya taasisi za elimu na mafunzo. Kwa hali hiyo, taasisi za elimu na mafunzo zinahitaji kumilikishwa kihalali ardhi ya kutosha kwa mahitaji ya sasa na maendeleo ya baadaye. Hivyo, ni muhimu mipango ya ardhi ikatoa kipaumbele katika kutenga ardhi ya kutosha kwa mahitaji hayo kwa ngazi zote. Aidha, kuna umuhimu kwa taasisi za elimu kuandaa mipango fanisi na endelevu ya matumizi ya ardhi zilizotengewa.

**Madhumuni**

Kuwa na ardhi ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya elimu na mafunzo.

## MATAMKO

*3.5.8 Serikali itahakikisha kuwa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya elimu na mafunzo yanazingatiwa katika mipango ya maendeleo ya ardhi nchini.*

*3.5.9 Serikali itahakikisha matumizi fanisi na endelevu ya ardhi yanazingatiwa katika taasisi za elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

**(j) Suala: Upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi za elimu na mafunzo.**

**Maelezo**

RASIMU

Hatua zote za mipango ya elimu zinategemea uwepo wa taarifa na takwimu sahihi na zenye ubora, zilizochanganuliwa kwa mujibu wa vigezo vyote muhimu. Ili kuweza kupata taarifa na takwimu kwa urahisi ni muhimu kuwa na mifumo fanisi, salama, rafiki na unganifu. Ingawa Serikali imeweka mifumo mbalimbali yenye taarifa na takwimu zinazohusu elimu na mafunzo, bado mifumo hiyo haikp unganifu. Aidha, usahihi wa baadhi ya taarifa na takwimu hauridhishi kutokana na changamoto katika ukusanyaji, uhakiki, uchambuzi na uhifadhi wake. Kuna umuhimu wa kuwa na mfumo madhubuti wa kukusanya, kuhakiki, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza takwimu na taarifa zote muhimu zinazohusu sekta ya elimu. Vilevile, kuna umuhimu wa kuimarisha upatikanaji wa taarifa zinazohusu elimu na mafunzo kwa kutumia tafiti za kisayansi.

**Madhumuni**

Kuwa na mfumo unganifu wa taarifa na takwimu zinazohusu sekta ya elimu.

## MATAMKO

*3.5.10 Serikali itahakikisha uwepo wa mfumo unganifu wa taarifa na takwimu zinazohusu elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*3.5.11 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha na kuwezesha kufanyika kwa tafiti na matumizi yake katika kuinua ubora wa elimu na mafunzo nchini.*

### 3.6 Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo



RASIMU

(b) **Suala: Ugharimiaji endelevu wa elimu na mafunzo**

**Maelezo**

Katika kutimiza azma ya Serikali ya kuwa na Taifa la watu walioelimika, ni muhimu kuwa na mfumo fanisi na endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imekuwa ikigharimia elimu na mafunzo katika ngazi zote. Hata hivyo, kutokana na ongezeko la mahitaji, na licha ya ongezeko la bajeti la mwaka hadi mwaka, bado kuna changamoto katika ugharimiaji wa elimu na mafunzo nchini. Changamoto hizo ni pamoja na fedha zinazotengwa katika bajeti ya Serikali kutotosheleza mahitaji, na hivyo kuathiri fursa za upatikanaji na ubora wa elimu. Kwa sababu hiyo, kuna umuhimu wa kuweka mfumo wenye vyanzo anuai na endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo.

**Madhumuni**

Kuwa na mfumo endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo.

## MATAMKO

*3.6.1 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuimarisha mfumo wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo wenye vyanzo anuai na endelevu katika ngazi zote.*

*3.6.2 Serikali itahakikisha kuwa ada na michango katika ngazi mbalimbali za elimu inazingatia misingi ya elimu bora na uendelevu wa uwekezaji katika sekta ya elimu.*

RASIMU

### 3.7 Masuala Mtambuka katika Elimu na Mafunzo

#### (a) Suala: Elimu ya mazingira

**Maelezo**

Elimu ni moja ya nyenzo muhimu katika kuhakikisha uwepo wa afya bora ya mazingira kwa maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Ongezeko la idadi ya watu na shughuli mbalimbali za kijamii na za kiuchumi zimechangia katika uharibifu wa mazingira nchini. Hivyo, kuna umuhimu wa kuimarisha utoaji wa elimu ya mazingira katika ngazi zote.

**Madhumuni**

Kuwa na wahitimu katika ngazi zote za elimu na mafunzo wenye uelewa na kuthamini umuhimu wa kutunza mazingira.

## TAMKO

*3.7.1 Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha kuwa maudhui kuhusu afya ya mazingira yanazingatiwa katika mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

#### (b) Suala: Magonjwa mbalimbali

**Maelezo**

Sekta ya elimu ni mojawapo ya sekta zinazoathirika na magonjwa mbalimbali. Magonjwa hayo yamesababisha kushuka kwa ubora wa elimu kutokana na vifo na mahudhurio duni ya walimu na

wanafunzi. Licha ya mitaala katika ngazi zote kusisitiza utoaji wa elimu ya afya, bado wanafunzi hawana uelewa wa kutosha wa mbinu za kujikinga dhidi ya magonjwa mbalimbali. Hivyo, kuna umuhimu wa kuimarisha elimu kuhusu magonjwa mbalimbali yanayoambukiza na yasiyoambukiza.

**Madhumuni**

Kuimarisha utoaji wa elimu kuhusu magonjwa mbalimbali yanayoambukiza na yasiyoambukiza katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

## TAMKO

*3.7.2 Serikali itajumuisha stadi za kujikinga na magonjwa mbalimbali yanayoambukiza na yasiyoambukiza katika mitaala ya elimu na mafunzo kwa ngazi zote kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika.*

**(c) Suala: Ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi katika utoaji wa elimu na mafunzo**

**Maelezo**

Elimu ni mojawapo ya eneo muhimu la ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ambapo sekta binafsi inashiriki kutoa elimu na mafunzo katika ngazi zote. Licha ya mchango mkubwa wa Serikali katika utoaji wa elimu, bado kuna umuhimu wa kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika jukumu hili. Aidha, ni muhimu kuimarisha ushirikishwaji wa wadau wote muhimu, ikiwemo wazazi na jamii, katika utoaji wa elimu. Kwa sababu hiyo, ni muhimu kwa Serikali kuweka mazingira wezeshi ili kuivutia sekta binafsi na wadau wengine kuongeza ushiriki wao katika utoaji wa elimu na

mafunzo.

**Madhumuni**

Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi na wadau wengine katika utoaji wa elimu na mafunzo

# MATAMKO

*3.7.3 Serikali itaimarisha ubia baina ya sekta ya umma, sekta binafsi na wadau wengine katika utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*3.7.4 Serikali itaimarisha ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

RASIMU

## SURA YA NNE

## MUUNDO WA KISHERIA

### 4.1 Utangulizi

Utekelezaji wa Sera utazingatia mfumo wa kisheria utakaowezesha wahusika kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Jukumu la sheria ni kuyapa nguvu ya kisheria matamko ambayo utekelezaji wake unahitaji uwepo wa sheria. Uwepo wa sheria utaondoa mkanganyiko na migongano ambayo ingeweza kujitokeza katika usimamiaji na utekelezaji wa masuala mbalimbali ya elimu nchini. Aidha, sheria zilizopo za taasisi zilizo chini ya Wizara au Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zinaweza kufanyiwa marekebisho au kufutwa kulingana na mahitaji. Vile vile, sheria mpya zinaweza kutungwa ikiwa sheria zilizopo itaonekana hazikidhi mahitaji katika kutekeleza baadhi ya matamko katika Sera. Hali kadhalika, sekta za umma na binafsi zinazoshughulikia utoaji wa elimu na mafunzo zitatakiwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayotolewa katika kuwezesha utekelezaji wa Sera.

### 4.2 Sheria za kusimamia elimu na mafunzo

Sheria zinazoweza kufanyiwa marekebisho au kufutwa ili kuendana na mahitaji ya matamko ya Sera ni kama zifuatazo:



RASIMU

a. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;

b. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;

c. Sheria ya Elimu, Sura ya 353;

d. Sheria ya Baraza la Mitihani la Tanzania, Sura ya 107;

e. Sheria ya Taasisi ya Elimu Tanzania, Sura ya142;

f. Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178;

g. Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346;

h. Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 129;

i. Sheria ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82;

j. Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, Sura ya 102;

k. Sheria ya Mfuko wa Elimu, Sura ya 412;

l. Sheria ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Sura ya 139;

m. Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 193;

n. Sheria ya Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania, Sura ya 314;

o. Sheria ya Tume ya Taifa ya UNESCO, Sura ya 348;

p. Sheria ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Sura ya 144;

RASIMU

q. Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia, Sura ya 226; na
r. Sheria ya Nguvu za Atomiki, Sura ya 188.

Vilevile, kwa sheria ambazo zipo chini ya mamlaka ya sekta nyingine na ambazo zinatekeleza baadhi ya matamko ya Sera, mamlaka husika inaweza kuzirekebisha au kuzifuta kulingana na mahitaji.

RASIMU

# SURA YA TANO
# MUUNDO WA KITAASISI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

## 5.1 Muundo wa Kitaasisi

Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo unahitaji muundo mahsusi wa kitaasisi katika ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi za chini za utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo.

## 5.2 Mgawanyo wa majukumu

Mgawanyo wa majukumu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ni kama ufuatao:

### 5.2.1 Ngazi ya Taifa

#### 5.2.1.1 Wizara yenye Dhamana ya Elimu na Mafunzo

Majukumu ya Wizara yenye dhamana ya Elimu na Mafunzo ni:

(i) Kutunga Sera ya Elimu na Mafunzo kwa ngazi zote;
(ii) Kuweka na kufuatilia utekelezaji wa mipango na bajeti ya maendeleo ya elimu na mafunzo nchini;
(iii) Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo;
(iv) Kujenga uwezo wa Wizara, taasisi na vyombo vilivyo chini ya Wizara kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake;
(v) Kutumia matokeo ya tathmini, tafiti na taarifa mbalimbali zinazohusu hali halisi ya utoaji wa elimu na

RASIMU

mafunzo ili Wizara iweze kutoa maamuzi yenye tija na yatakayoongeza ufanisi katika utekelezaji wa mkakati wa Sera;

(vi) Kubuni na kutekeleza miradi mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya elimu na mafunzo nchini;

(vii) Kuweka viwango vya ubora wa elimu na mafunzo na kusimamia utekelezaji wake;

(viii) Kuandaa muundo fanisi wa kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa Sera na kumshauri Waziri kuhusu utekelezaji wake katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo.

Katika utekelezaji wa Sera, sheria, kanuni, miongozo na taratibu za utoaji wa elimu na mafunzo, Wizara yenye dhamana ya Elimu na Mafunzo itazishirikisha wizara nyingine, taasisi na wadau wanaojihusisha na utoaji wa elimu na mafunzo nchini.

#### 5.2.1.2 Wizara yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itakuwa na jukumu la kuratibu mipango, bajeti, usimamizi na uendeshaji wa elimu kwa ngazi ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

#### 5.2.1.3 Wizara zenye Dhamana ya Sekta Nyingine

Wizara nyingine zitahusika katika utekelezaji wa Sera kwa kuhakikisha uwepo wa mipango na bajeti inayozingatia utekelezaji wa maelekezo ya Sera. Aidha, Wizara hizo hazitakuwa na mamlaka ya moja kwa moja ya kutoa maelekezo kwenye taasisi za elimu na mafunzo isipokuwa kwa kupitia Wizara yenye dhamana ya elimu.

#### 5.2.1.4 Taasisi na Mamlaka Mbalimbali za Kusimamia Utoaji wa Elimu na Mafunzo

Taasisi na mamlaka simamizi zitakuwa na jukumu la kutoa ithibati, kuthibiti na kusimamia masuala mbalimbali ya elimu na mafunzo nchini kulingana na majukumu yake kama yalivyoainishwa kisheria. Mamlaka hizo zitakuwa huru na zenye kauli ya mwisho, isipokuwa pale tu zitakapoelekezwa vinginevyo na Waziri mwenye dhamana ya elimu na mafunzo. Aidha, katika kutekeleza majukumu yake, mamlaka hizo zitashirikiana kwa karibu na wizara, idara, taasisi na wadau wote muhimu.

#### 5.2.1.5 Taasisi na Bodi Mbalimbali za Kitaalamu

Taasisi na Bodi zenye wajibu na masuala mbalimbali ya kitaalamu zitawajibika katika masuala ya utaalamu baada ya wanafunzi kumaliza masomo yao kwenye taasisi za elimu na mafunzo husika. Aidha, Taasisi na Bodi hizo zitawajibika kuzishauri mamlaka mbalimbali zinazosimamia utoaji wa elimu na mafunzo nchini kwenye masuala ya viwango vya elimu na mafunzo yatolewayo. Hata hivyo, Taasisi na Bodi za kitaalamu hazitakuwa na mamlaka ya moja kwa moja ya kutoa maelekezo kwenye taasisi za elimu na mafunzo isipokuwa kwa kupitia kwenye mamlaka rekebu (taasisi simamizi au elekezi za elimu) za taasisi hizo.

### 5.2.2 Ngazi ya Mkoa

Jukumu la usimamizi wa utekelezaji wa Sera katika ngazi ya mkoa litakuwa la Afisa Elimu wa Mkoa husika. Afisa Elimu Mkoa atakuwa na jukumu la kutoa taarifa na ushauri kwa mamlaka

husika kuhusu utekelezaji wa Sera na maendeleo ya elimu na mafunzo katika ngazi hiyo.

### 5.2.3 Ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

Jukumu la usimamizi na utekelezaji wa Sera katika ngazi ya Halmashauri litakuwa la Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya usimamizi wa Afisa Elimu wa Halmashauri husika. Afisa Elimu wa Halmashauri atakuwa na jukumu la kuandaa mipango na bajeti na kusimamia uendeshaji wa shule za elimu ya awali, msingi na sekondari kwa kuzingatia maelekezo ya Sera. Afisa Elimu wa Halmashauri atakuwa na jukumu la kutoa taarifa na ushauri kwa mamlaka husika kuhusu utekelezaji wa Sera na maendeleo ya elimu na mafunzo katika ngazi hiyo.

Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitahusika katika uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wa shule za elimu ya awali, msingi, sekondari, vituo vya elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi katika maeneo wanayosimamia kulingana na maelekezo ya Sera. Vilevile, zitawajibika kutoa taarifa ya utekelezaji wa Sera kwa mamlaka husika.

Mamlaka za Serikali za Mitaa pia zitasimamia utekelezaji wa Sera kwa kufuata sheria, kanuni, miongozo na taratibu za usimamizi na uendeshaji wa shule za Serikali na zisizo za Serikali. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mamlaka zitatakiwa kushirikiana na Walimu Wakuu wa shule za msingi na Wakuu wa shule za sekondari za Serikali na zisizo za Serikali, n a mashirika na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali katika ngazi hizo.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zitawajibika pia kufanya uthibiti wa

ubora wa elimu na mafunzo wa shule zilizoko katika maeneo yao kulingana na miongozo itakayotolewa na taasisi na mamlaka mbalimbali za kusimamia utoaji wa elimu na mafunzo nchini katika ngazi na mfumo husika. Vilevile, Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo zitawajibika kutoa taarifa kwenda katika mamlaka husika ya usimamizi wake.

### 5.2.4 Shule na Vyuo

Wakuu wa shule na vyuo watasimamia na kutekeleza Sera kwa kuzingatia maelekezo ya Sera. Aidha, watawajibika kutoa taarifa za utekelezaji wa Sera katika taasisi zao kwa mamlaka husika.

## 5.3 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Sera ni jukumu la Wizara yenye dhamana ya Elimu na Mafunzo. Utekelezaji wa Sera utafafanuliwa katika Mkakati wa Utekelezaji wa Sera. Wizara yenye dhamana ya Elimu na Mafunzo itakusanya, kuchambua, na kuunganisha taarifa za utekelezaji wa maeneo mbalimbali. Wadau muhimu watawajibika kutoa taarifa stahiki kwa Wizara ili kufanikisha ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya utekelezaji wa Sera. Wizara itaandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera ambao utaonesha viashiria, vigezo na muda wa tathmini.

## 5.4 Mwisho

Madhumuni ya Sera hii ni kutoa mwongozo wa jumla wa uendeshaji wa elimu na mafunzo kwa kuzingatia mipango na mikakati ya maendeleo ya Taifa na mabadiliko ya ulimwengu

katika nyanja za uchumi, sayansi na teknolojia. Lengo kuu la Sera ni kuinua ubora wa elimu utakaowezesha kuandaa Watanzania wa kutosha, wenye maarifa, stadi na mwelekeo chanya walio tayari kujenga Taifa lenye uchumi shindani na endelevu. Sera hii itaambatana na Mkakati wa Utekelezaji utakaotoa mwongozo wa namna Matamko ya Sera yatakavyotekelezwa.

**Elimu bora na yenye tija kwa maendeleo ya Taifa inawezekana, wote tutekeleze wajibu wetu**

RASIMU